SportPesa
TZS. 517,350,800
CHEZA USHINDE JACKPOT
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**DPP** afuta kesi ya Lissu, sasa abaki na kesi tatu Kisutu

UKURASA 5



**Hatima ya Sterling mashakani England**

UKURASA 21


# Nipashe

Alhamisi Septemba 23, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580712

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Benki ya Dunia kutatua tatizo la ajira nchini

• **Kigogo** wake ateta na Rais Samia Marekani, aahidi kukuza uchumi... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Rais wa Benki ya Dunia (WB), David Malpass, walipokutana katika ufunguzi wa mkutano wa 76 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UN), jijini New York, nchini Marekani juzi. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO


UKURASA WA 3
**MWIGULU AWAPA 'MENO' WAKAGUZI WA NDANI**
WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amewaonya...

UKURASA WA 5
**TAHADHARI MAGONJWA YASIYOAMBUKIZA**
IDADI ya watu wanaoathirika na magonjwa yasiyoambukiza (NCDS)...

UKURASA WA 19
**MUHIMBILI YATUMIA BIL. 60/- MISAMAHA MATIBABU**
HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH), imetumia zaidi ya Sh. bilioni...


## Jeneza lakutwa shambani lina ndizi

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


RIPOTI MAALUM



## Rugemalira alivyoibua mjadala haki ilikojificha

UKURASA 4

**MICHEZO** **NABI: YANGA SC TUTAWEKA REKODI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipata maelezo kutoka kwa Meneja Uendeshaji wa kiwanda cha kusafisha madini ya dhahabu cha Geita Gold Refinery cha mjini Geita, Ahmet Lyal (kushoto), alipotembelea kiwanda hicho, jana. Kulia ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa kiwanda hicho, Sarah Masasi. **PICHA: OWM**

# Benki ya Dunia kutatua tatizo la ajira Tanzania

**Na Mwandishi Maalum**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameshiriki ufunguzi wa mjadala mkuu katika Mkutano wa 76 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa ambao wakuu wa nchi na serikali walishiriki na kuanza kutoa hotuba zao.

Vilevile, Rais Samia amekutana na kufanya mazungumzo na Rais wa Benki ya Dunia (WB), David Malpass, aliyemshukuru mkuu wa nchi huyo kwa jitihada za kupambana na UVIKO-19 nchini.

Taarifa iliyotolewa na Ikulu jana, ilibainisha kuwa Malpass alimhakikishia Rais Samia kuwa Benki ya Dunia itaendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika kukuza uchumi kupitia mabadiliko ya kidijitali kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Tanzania imeripotiwa na Shirika la Kazi Duniani (ILO) kuwa miongoni mwa nchi zinazokabiliwa na tatizo la uhaba wa ajira kwa wananchi wake, hususan vijana.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) haiko nyuma katika tathmini ya tatizo hilo kitaifa.

CAG, Charles Kichere, kupitia ripoti ya 2019/20 iliyowasilishwa bungeni Aprili, mwaka huu, anasema kupungua uwekezaji mpya kumekwaza ajira.

Anabainisha miradi mipya kwenye Kituo cha Uwekezaji (TIC) ilipungua kwa wastani wa nusu na ndiyo ulikuwa uhalisia wa mwenendo wa ajira nchini miaka mitano iliyopita.

CAG anasema ndani ya kipindi hicho, ajira zilipungua kutoka waajiriwa 63,223 mwaka 2015/16 hadi waajiriwa 32,115 mwaka 2019/20, sawa na asilimia 48.

Katika mazungumzo yao hayo, Rais Samia aliishukuru Benki ya Dunia kwa mchango wake kwa Tanzania katika huduma za jamii pamoja na mapambano dhidi ya UVIKO-19.

Vilevile, Rais Samia alikutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Biashara Duniani (WTO), Ngozi Okonjo-Iweala, viongozi hao walizungumzia kuwezesha biashara kwa kuimarisha upatikanaji wa chanjo, usimamizi wa uvuvi na kilimo.

Rais Samia pia alishiriki Mkutano Maalum wa Wakuu wa Nchi na Serikali Wanawake wanaoshiriki mkutano wa 76 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa na kumhakikishia Rais wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, Abdulla Shahid, kuwa Tanzania itaendelea kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kunakuwapo na usawa wa kijinsia licha ya vikwazo vinavyojitokeza.

Alisema kuwa tangu amekuwa Rais, ameendelea kuteua viongozi wanawake katika nafasi mbalimbali ambazo hazijawahi kushikwa na wanawake ili kuondokana na dhana ya kuwa kuna nafasi ambazo wanawake hawawezi.

"Hivi karibuni nimemteua Waziri wa Ulinzi ambaye amekuwa mwanamke wa kwanza kushikilia nafasi hiyo nchini mwetu, ili kuondokana na dhana kuwa wanawake wanaweza nafasi fulani tu," alisema Rais Samia.

Rais alisema kuwa hivi karibuni aliunda timu ya wataalamu ambao kwa sasa wanaangalia namna bora kwa Tanzania kufanikiwa katika kupata usawa wa kijinsia wakati wa uongozi wake na timu hiyo itakuja na mapendekezo kadhaa ya kuwainua wanawake katika vita dhidi ya umaskini.

Maeneo ambayo timu hiyo inapitia ni pamoja na marekebisho ya sheria kandamizi, sera na mikakati ya kuwasaidia wanawake katika kupata fursa kwenye nyanja mbalimbali ikiwamo ajira, elimu na nyinginezo za kuwainua kiuchumi kama vile kumiliki ardhi, kupata mikopo na nafasi za uongozi.

Rais Samia pia alitoa wito kwa washiriki wenzake katika kikao hicho kutotoa fursa kwa ugonjwa wa virusi vya corona kuwa kikwazo cha kuzuia mafanikio kwenye usawa wa kijinsia na kusisitiza kuwa ili malengo 17 ya Maendeleo Endelevu kufanikiwa, lengo namba 5 kuhusu usawa wa kijinsia ni lazima lifanikiwe.

# PM aridhishwa GGML kuajiri Watanzania 5,000

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ameipongeza Kampuni ya Uchimbaji Dhahabu Geita (GGML) kwa kutoa ajira zaidi ya 5,000 kwa Watanzania, huku asilimia zaidi ya 83 ya uongozi wa kampuni hiyo wakiwa Watanzania.

Waziri Mkuu alitoa kauli hiyo jana mkoani Geita wakati akizindua maonyesho ya nne ya teknolojia za uchimbaji madini mkoani Geita.

Alisema licha ya GGML kushirikiana na serikali na kutoa ajira za kutosha kwa Watanzania wengi, bado kumekuwapo na baadhi ambao sio waamini jambo ambalo linatakiwa kushughulikiwa.

Kutokana na hali hiyo, amewaagiza maofisa madini mkoani humo, kushughulikia wafanyakazi wote ambao si waadilifu.

Aidha, ametoa wito kwa Watanzania kuchangamkia fursa katika maeneo ambayo madini mbalimbali yanagundulika ili kujikwamua kiuchumi.

Alisema Tanzania ni nchi yenye madini mengi mbali na dhahabu ambayo inachimbwa maeneo mengi.

"Huko Ulanga tumegundua ghraphite zaidi ya tani milioni 235, Kyerwa tuna madini ya tin ya kutosha zaidi ya tani bilioni nne zitachimbwa zaidi ya miaka 70 wakati madini ya bati yamepanda thamani kubwa baada ya wizara kusimamia, kg 6,000, sasa ni 34,000 kwa kilo.

"Nimewaambia wanaKerwa, Bukoba wajipange... pesa ipo Tanzania bado ni tajiri. Nitoe rai kwa vijana kuchangamkia fursa zilizopo katika maeneo yenye miradi ya madini," alisema.

Makamu wa Rais wa GGML, Simon Shayo, alisema mbali na ulipaji wa mapato ya Serikali na uwekezaji kwenye jamii, Kampuni hiyo imetoa ajira kwa Watanzania zaidi ya 5,000 ikiwa ni pamoja na wale wanaofanya kazi chini ya makandarasi wetu.

Alisema hadi kufikia sasa takriban asilimia 98 ya wafanyakazi wa GGML na asilimia 83 ya menejimenti ni Watanzania.

Katika hatua nyingine, Alisema imedhamiria kuhakikisha kuwa rasilimali za nchi zinachangia katika kuinua uchumi wa Watanzania.

"Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, anawaahidi kuendelea kuchukua hatua madhubuti katika kulinda na kuendeleza rasilimali hizi ili ziweze kuwanufaisha na kuwaletea maendeleo Watanzania wote, tuendelee kuunga mkono."

Alisema serikali ya itaendelea kufanya marekebisho ya baadhi ya kanuni na taratibu zinazosimamia uchimbaji na biashara ya madini kwa lengo la kuwezesha wananchi na wadau mbalimbali kushiriki ipasavyo katika uchumi wa madini na kuongeza uwekezaji.

Hata hivyo, aliwataka wadau wa sekta ya madini nchini wazingatie na wafuate sheria, kanuni, taratibu na miongozo inayosimamia sekta hiyo ili kuondoa usumbufu na kurahisisha utendaji wa shughuli zao na serikali kwa manufaa ya pande zote.

Waziri Mkuu amesema serikali imeendelea kuweka mikakati ya kuimarisha Taasisi ya Jiolojia Tanzania (GST) na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) ili ziweze kutoa huduma bora na nafuu kwa wachimbaji wadogo ikiwa ni pamoja na uchorongaji wa miamba ili kujua uwepo na wingi wa mashapo.

Kwa upange wake, Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alisema wizara itaendelea kusimamia biashara ya madini nchini ili kuhakikisha ndoto ya Rais Samia ya kutaka kuona Tanzania inakuwa kitovu kikubwa cha biashara ya madini inatimia.

Naye Rais wa Muungano wa Wachimbaji Wadogo Tanzania, John Mbina, aliipongeza serikali kwa namna inavyosimamia ukuaji wa sekta ya madini nchini.

## HABARI KITAIFA



Jeneza lenye mkungu wa ndizi ndani, likiwa limetelekezwa shambani katika kijiji cha Kiwawa, Kata ya Imbaseny, wilayani Arumeru, mkoani Arusha jana, kitendo kilichozua taharuki kwa wakazi wa eneo hilo. **PICHA: TUMAINI MAFIE**

# Jeneza lakutwa shambani likiwa na ndizi ndani yake

**Na Tumaini Mafie,**
ARUMERU

TAHARUKI imewakumba wakazi wa Kijiji cha Kiwawa Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha, baada ya jeneza kukutwa shambani likiwa limewekwa ndizi ndani yake.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya mashuhuda wa tukio hilo walisema awali shamba hilo lilikuwa na mgogoro, kwamba inadaiwa waliokuwa wakigombania shamba hilo ndiyo walioweka jeneza hilo.

Walieleza kuwa jeneza hilo, lilibainika kuwa na mkungu wa ndizi ndani huku kwenye msalaba zikionekana tarakimu zilizoandikwa 1-100.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kiwawa, Ernest Palangyo, alikiri kutokea kwa tukio hilo katika kijiji chake, huku akieleza kwamba awali kulikuwa na mgogoro katika shamba hilo.

Alisema ni tukio la kushangaza kutokea katika kijiji chake, kwamba ni mara ya kwanza kutokea na kusababisha taharuki kwa wakazi wa kijiji hicho.

Mmoja wa watoto wa mmiliki wa shamba hilo, Abraham Pallangyo, alisema shamba hilo halina mgogoro bali ni mgogoro wa kutengeneza.

"Shamba hili halijawahi kuuzwa maana hakuna nyaraka zozote zinazoonyesha liliwahi kuuzwa. Bali ni mtu tu aliamua kutishia na ikabidi tukaenda mahakamani, lakini hawakuweza kuonyesha andiko lolote kuwa shamba limeuzwa. Hata serikali ya kijiji haijawahi kupelekewa taarifa ya kuuzwa wala kununuliwa kwa shamba hili," alisema Pallangyo.

Alisema kwa sasa wanasubiri maelekezo ya nini wanatakiwa kufanya baada ya jeneza hilo kuwekwa katika shamba lao.

"Tunatamani kuona polisi wakitupa mwongozo nini kifanyike baada ya wao kufanya uchunguzi kama itawapendeza, lakini pia tukipata maelekezo katika ulimwengu wa roho tutatekeleza," alisema Pallangyo.

Shuhuda mwingine wa tukio hilo, Emanuel Sarakikya, alisema alifika eneo la tukio baada ya kuona jeneza, alilifunua na kuangalia kilichopo ndani ndipo akakutana na mkungu wa ndizi kitendo ambacho alisema ni cha kushangaza.

Mmoja wa wanafamilia wanaomiliki shamba hilo, Eliarimisa Pallangyo, alisema amekuwa akilima muda mrefu katika shamba hilo bila tatizo lakini Julai 15, mwaka huu alifika shambani na kuanza kuvuna maharagwe, ndipo akakutana na umati wa watu wakiwa shambani.

# Mwigulu awapa 'meno' wakaguzi wa ndani

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amewaonya wakuu wa mashirika ya umma na taasisi binafsi nchini kuacha tabia ya kuwaingilia wakaguzi wa ndani katika utekelezaji wa majukumu yao.

Dk. Mwigulu alitoa ovyo hilo jana jijini Arusha, wakati akifungua mkutano wa nane wa Taasisi ya Wakaguzi wa Ndani Tanzania (IIA).

Alisema wakaguzi wa ndani wamekuwa msaada mkubwa katika maendeleo ya nchi na wamekuwa wakiwasisitiza kuangalia kasoro zote zinazojitokeza kabla ya wakaguzi wa nje.

"Wakaguzi wa ndani hasa wa serikali wamekuwa na mchango mkubwa wa maendeleo kwa kuwa wapo ndani ya ofisi za umma na wanaweza kuzuia upotevu wa fedha katika mashirika na taasisi zao," alisema Mwigulu.

Alisema wakati Rais Samia Suluhu Hassa akipokea ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), alitoa mwelekeo wa serikali yake, kuwa wakaguzi wote wa hesabu za serikali hawapaswi kuficha kitu chochote bali wanatakiwa kukagua kwa ujasiri kwa ajili ya kulinda fedha za wananchi.

"Kiongozi wa taasisi yoyote hapaswi kuwatisha wale ambao wanaotakiwa kusimamia ukaguzi wa fedha za walipakodi wa Tanzania, hivyo nasisitiza kuwa kila kiongozi anatakiwa kuzingatia kauli ya Rais Samia akimweleza CAG kwamba hatakiwi kupepesa macho wakati wa ukaguzi, bali anapaswa kuwa wazi na jasiri.

"Kauli ya Mheshimiwa Rais ni maelekezo kwa kila yeyote anayeitumikia serikali hii, hivyo sitarajii kwamba atatokea kiongozi au mtu atakayekwenda kinyume cha agizo hili," alisema Mwigulu.

Aidha alisema serikali imepanga kutoa fedha nyingi kwa ajili ya kupeleka kwenye miradi ya maendeleo na matarajio ya Watanzania ni kuona matokeo chanya ya hizo fedha, hivyo mafunzo waliyopewa wakaguzi hao yatasaidia kwenda kuzisimamia vizuri na kudhibiti mianya ya wizi wa fedha hizo.

"Sisi kama Wizara ya Fedha na Mipango tutaendelea kushirikiana kwa ukaribu na taasisi hii waweze kutimiza majukumu yao ipasavyo, na watumishi wengi wa kada hii wafanikiwe kupata mafunzo haya na kubadilishana uzoefu," aliongeza.

Mkurugenzi Mkaguzi wa Benki ya Maendeleo Tanzania (TIB), Christine Mbonya, alisema maagizo yaliyotolewa na waziri huyo kwa wakaguzi wa ndani watakwenda kuyafanyia kazi kwa kuwa amewapa nguvu ya kufanya kazi kwa bidii, kwa maarifa zaidi na kwa kutokuogopa.

Rais na Mwenyekiti wa IIA, Anna Victor, alisema:

"Tamko hili tumelipokea kama wazo chanya kwa kuwa linatutia moyo sisi tuendelee kusonga mbele zaidi kwa kuwa kwa muda mrefu tumekuwa tuna tatizo ambalo limekuwa likizuia katika utendaji kazi wetu kwa uhuru."


**Summons to appear (O.VR.20 (1) of (CPC)**
**(Substituted Service)**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR-ES-SALAAM**

**LAND CASE NO 75 OF 2021**

**HALIMA MAKWAI A ..................................................PLAINTIFF**

**VERSUS**

**COMMISSIONER FOR LANDS & MINISTRY OF OF LANDS,HOUSING AND HUMAN SETTLEMENT DEVELOPMENT & OTHERS........................DEFENDANTS**

**TO:**

**JEREMIA C KILEMBE**
**PLOT NO 671 MBEZI BEACH**
**DAR-ES-SALAAM**

**WHEREAS:** The above named PLAINTIFF. has instituted the SUIT against you, you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or agent duly authorized on 19th day of OCTOBER, 2021 at 09:00 AM before Hon. DR.T.MWENEGOHA JUDGE (Chamber No. 06) in the morning to answer the said SUIT and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your DEFENCE,

**TAKEN NOTICE** that, in default of your appearance on that day the SUIT will be heard and determined in your absence.

GIVEN UNDER MY hand and the seal of this Court, this 9TH day of september 2021

DEPUTY REGISTRAR

216472401

## WIKI MOJA URAIANI...

# Rugemalira afukua mjadala darasa la haki ilikosimama

## ■Adumisha msimamo wake, aongeza mpya
## ■Wanasheria wanyanyuka kuhoji vifungu

**Na Sanula Athanas**

ILIKUWA saa sita mchana, Alhamisi ya wiki iliyopita, vilio vya furaha na nderemo ghafla vikatawala viunga vya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam.

Wakati wasiojua wakitekwa na mshangao wa "nini kimetokea?" majibu ya haraka yanawarejea kutoka kwa wanafamilia, ndugu na jamaa wa mfanyabiashara James Rugemalira, wakimshuhudia kwa furaha sasa yuko huru.

Ni siku ambayo kesi ilipangwa kwa ajili ya kutajwa mbele ya Hakimu Mkazi Huruma Shaidi, lakini ghafla muktadha wa shauri unageuka na kufikisha mwisho wa siku zake gerezani Segerea ambazo zilishatimu 1,550.

Kwa hesabu rahisi, hiyo ni miaka minne na miezi mitatu, yaani tangu Juni 19, 2017 siku aliyopandishwa kizimbani kwa mara ya kwanza kusomewa mashtaka ya Uhujumu Uchumi na akahamishiwa kwenye makazi hayo mapya.

Ni hoja ya kisheria iliyowasilishwa mbele ya Hakimu Mkazi Shaidi kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), kwamba hana nia ya kuendelea na mshtakiwa huyo.

Kabla Hakimu Shaidi hajatoa uamuzi, Wakili wa Serikali, Grace Mwanga, anadai mahakamani kwamba DPP anatumia mamlaka yake chini ya Kifungu cha 91(1) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kuiomba mahakama imwachie huru.

Kifungu hicho kinatamka: "Katika sheria yoyote ya jinai na katika hatua yoyote ile kabla ya hukumu au uamuzi, kama itakavyokuwa, Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza kuweka 'nolle prosequi', aidha kwa kueleza mahakamani au kuiambia mahakama husika kwa maandishi kwa niaba ya Jamhuri kuwa mwenendo hautaendelea.

"Na baada ya hapo mtuhumiwa ataachiwa mara moja kuhusiana na shtaka ambalo 'nolle prosequi' imewekwa na kama amepelekwa gerezani atatakiwa kuachiwa, au kama yuko chini ya dhamana, wadhamini wake watakoma kuwa wadhamini.

"Lakini kuachiwa huko kwa mtuhumiwa hakutachukuliwa kama kizuizi cha mashtaka mengine dhidi yake kwa kutumia maelezo hayo hayo."

Ndipo Hakimu Shaidi anamwachia huru Rugemalira na ghafla analakiwa nje ya mahakama na wadau wake ambao nao bila ya kupoteza muda, wanaanza safari ya kuongozana naye hadi eneo la Makongo Juu, umbali wastani wa Km 18 kutoka Kisutu. Huko wanafikia kwenye Kanisa Katoliki Makongo Juu anakoanza maisha mapya kwa kushiriki Ibada ya Shukrani, kisha anaelekea hadi nyumbani kwake jirani na eneo hilo.



Mfanyabiashara James Rugemalira (mwenye kanzu) akilakiwa na familia yake, ndugu na jamaa baada ya kuachiwa huru katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Alhamisi ya wiki iliyopita. **PICHA: MTANDAO**

Wakati wa ibada, Paroko wa Kanisa hilo, Padri Joseph Massenge, anamtaka Rugemalira kusamehe kwa yote yaliyofanyika dhidi yake, naye akiitikia kwa sentensi moja "sina kinyongo na mtu, nimewasamehe wote".

**KUTONYOA MIAKA MINNE**

Siku tatu baadaye, Rugemalira anarejea kanisani kuungana na waumini wenzake kwa misa ya Jumapili na safari hii anatoa ufafanuzi kuhusu uamuzi wake wa kutonyoa nywele na ndevu kwa kipindi chote alichokuwa mahabusu gerezani.

Akizungumza kwa sauti ya chini, uso wake ukionesha wenye furaha, mtulivu na kuna baadhi ya hatua anasita, Rugemalira anasema:

"Juzi (Alhamisi) nilipokuja (kanisani) kumshukuru Mungu baada ya kuachiwa huru, nilimwomba Baba Paroko amwambie 'baby' (mkewe) asininyoe hizi ndevu maana alitaka kuninyoa.

"Ninataka niwashuhudie kwamba hizi nywele na ndevu sijawahi kunyoa tangu niingie gerezani (mahabusu) miaka yote hiyo...

"Hizi nywele na picha mnayoiona hapa... (anasita kuongea) inazungumza maneno mengi kuliko hata kauli yangu. Ninawashukuru kwa sala na maombezi yenu, tuko pamoja," anatamka Rugemalira na kupokewa kwa mwitikio wa shangwe kanisani.

**FAMILIA GIZANI**

Mke wa Rugemalira, Benedicta Rugemalira, anamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan na serikali kwa kumwachia huru mume wake, akisisitiza uamuzi huo umeiondoa familia hiyo kwenye giza lililotanda kwa miaka minne.

Anasema walikuwa hawaelewi kama kuna siku ingetokea mume wake huyo angekuwa huru kutokana na msimamo aliokuwa ameuweka.

"Tulikuwa hatuelewi cha kufanya maana wapo waliokuwa wanasema akubali alipe hizo fedha ili atoke, lakini mwenyewe alisimama imara na kusema hawezi kusema uongo na yuko tayari kwa lolote kuthibitisha ukweli wake.

"Tuna kila sababu ya kumshukuru Mungu kwa kumwezesha Mzee Rugemalira kutoka gerezani, ukweli ni kwamba tulikuwa kwenye giza zito," anasema.

Paroko wa Parokia hiyo, Padri Massenge, anamtaja Rugemalira ni mfano bora kwa waumini wake kusimamia ukweli unaotiliwa mkazo kwenye mafundisho ya kiroho.

"Mnatakiwa kuiga mfano wa maisha haya, jitoe sadaka, simamia ukweli. Kama unasimamia ukweli, hivyo hivyo hata kama utakufa, simamia ukweli.

"Mzee (Rugemalira) ninakupongeza umesimamia ukweli mpaka dakika ya mwisho na hivyo ndivyo Mungu anavyotaka! Mungu anamjalia yule anayesimama katika haki na haya ndio maisha tunayotakiwa.

"Mama (mke wa Rugemalira) amenifuata mara nyingi kuniambia nimwombe askofu aongee na mzee (Rugemalira). Mimi nikwambia 'siende kokote, yule mzee ni 'hero' (shujaa), hatabadilika'. Kweli sikwenda.

"Nilikwenda kumtembelea gerezani mara nne, siku zote amebaki na msimamo wake licha ya magumu aliyopitia katika kipindi chote hicho, akasimamia kile alichoamini kuwa hajaiba na yuko tayari kutoa ushirikiano," anasema.

**KILICHOMKUTA**

Rugemalira, Mkurugenzi wa VIP na mmiliki mwenza wa zamani wa kampuni ya kufua umeme ya IPTL, alikabiliwa na mashtaka 12 ya jinai mahakamani, likiwamo dai la kutakatishaji fedha na kuisababishia serikali hasara ya Dola za Marekani milioni 22.198 na Sh. bilioni 309.461.

Kila mara kesi hiyo ilipotajwa, upande wa mashtaka uliomba iahirishwe ukidai upelelezi ulikuwa haujakamilika, hivyo kumfanya Rugemalira na wenzake wawili kuendelea kubaki mahabusu kutokana na shauri hilo kutokuwa na dhamana kisheria.

Februari 13, mwaka jana, Rugemalira aliwasilisha hoja maalum mahakamani kumwomba DPP amwondoe katika kesi hiyo, akidai hakuna kigezo cha kisheria kumshikilia.

Alidai mahakamani kwamba alishawasilisha barua kwa Kamishna wa Mamlaka ya Mapato (TRA) kupitia mjumbe wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) aliyetembelea gerezani.

Kwa mujibu wa Rugemalira, barua hiyo ilikuwa na ufafanuzi wa jinsi Benki ya Standard Chartered ya Hong Kong ilivyokwepa kodi na ndiyo iliyopaswa kujumuishwa kwenye kesi hiyo na sio yeye.

Pia alidai alishawasilisha taarifa kwa taasisi tisa husika, ikiwamo Idara ya Usalama wa Taifa (TISS), akimtaka DPP awasilishe hati ya kuachiwa kwake na asipofanya hivyo, yeye atawasilisha hoja ya kuiomba mahakama imwondoe katika kesi hiyo.

Mnamo Juni 15, mwaka huu, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, ilimwachia huru mshtakiwa mwenza katika kesi hiyo, Mkurugenzi wa IPTL, Herbinder Seth, kwa masharti ya kutotenda makosa tena na kuwa chini ya uangalizi kwa mwaka mmoja, baada ya kukiri makosa na kukubali kulipa Sh. bilioni 26.9.

Mshtakiwa wa tatu katika kesi hiyo ni Joseph Mwakandege ambaye kesi yake inatarajiwa kutajwa leo. Katika kesi ya msingi ya Uhujumu Uchumi Na. 27 ya mwaka 2017, Makandege anakabiliwa na mashtaka matano likiwamo la kuisababishia serikali hasara ya Dola za Marekani 980,000, pia yapo ya utakatishaji wa fedha.

**HAKI ILIKOSIMAMIA**

Uamuzi wa DPP kutoendelea na kesi dhidi ya Rugemalira, unawaibua wadau wa sheria na haki za binadamu wanaopaza sauti upya kudai mabadiliko ya sheria husika katika eneo hilo.

Hapo hoja yao inaangukia moja kwa moja kwenye dai la muda wa ukomo wa upelelezi katika kesi zilizoko mahakamani na mazingira yanayoendana na hatua hiyo ya kisheria.

Vilevile, wadau hao wananyooshea kidole mamlaka makubwa kupitiliza ya DPP, wakipendekeza apunguziwe nguvu, ili kusiwapo mianya inayosababisha watu kukaa mahabusu kwa muda mrefu na baadaye kuachiwa huru kwa sababu mbalimbali, ikiwamo kukosekana kwa ushahidi.

Anna Henga ni Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), anaiambia Nipashe kwamba hivi sasa ni wakati mwafaka wa kuirekebisha sheria ili kuwapo muda maalum ambao uchunguzi wa shauri la jinai unapaswa uwe umemilika.

Mdau huyo wa sheria, anatoa mfano ukomo huo unaweza kuwa ni miezi mitatu na ukishindwa kufanikisha, basi mtuhumiwa apewe haki yake ya kubaki huru.

"Kama kuna muda fulani wa kuchunguza, timu ya uchunguzi ya DPP itakuwa makini kuchunguza kesi husika. Sheria ikisema upelelezi lazima ukamilike ndani ya miezi mitatu kwa mfano, siyo mbaya," anasema.

Katika ufafanuzi wake, anarejea shauri la mshtakiwa Rugemalira, akilipa tafsiri anayoibatiza 'machungu nusu na furaha nusu'.

Hapo anaipa ufafanuzi kwamba kwa upande mmoja wapendwa wake wametabasamu kumwona yuko huru, lakini sura ya pili ni huzuni kutokana na kudumu gerezani miaka minne na kisha inatamkwa kisheria 'hakuna haja ya kuendelea na kesi hiyo'.

**ITAENDELEA KESHO**

## HABARI KITAIFA

# DPP afuta kesi ya Lissu

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam imemwachia huru Mbunge wa zamani wa Singida Mashariki, Tundu Lissu, na wenzake watatu waliokuwa wakikabiliwa na kesi ya uchochezi baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuona hana nia ya kuendelea kuwashtaki.

Kesi hiyo imefutwa na kufanya idadi ya kesi zinazomkabili Lissu katika mahakama hiyo kubakia tatu. Uamuzi huo ulitolewa jana katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Joseph Lwambano.

Wakili wa Serikali, Ashura Mzava, alidai kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa.

Hata hivyo, alidai upande wa Jamhuri unaomba kuwasilisha hati ya nolle kutoka kwa DPP chini ya kifungu cha 91(1) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA) kwamba hana nia ya kuendelea kuwashtaki washtakiwa.

Hakimu alisema kwa kuwa Jamhuri wameona hawana nia ya kuendelea kuwashtaki washtakiwa, mahakama yake inawaachia huru.

"Mahakama yangu chini ya kifungu hicho inawaachia huru washtakiwa dhidi ya mashtaka yanayowakabili washtakiwa wote wanne," alisema Hakimu Lwambano.

Kesi hiyo ilikuwa hatua ya kusikilizwa ushahidi wa Jamhuri. Hata hivyo, baada ya Lissu kujeruhiwa kwa risasi na kwenda kwenye matibabu, kesi hiyo na nyingine zinazomkabili zilisitishwa kutajwa mpaka mshtakiwa atakapopona na kufika mahakamani.

Mbali na Lissu, washtakiwa wengine ni, wahariri wa gazeti la Mawio, Simon Mkina na Jabir Idrisa na mchapaji wa magazeti, Ismail Mehboob. Akizungumza na Nipashe jana, Mehboob alisema tangu afikishwe mahakamani mwaka 2016 kwa tuhumu zilizofutwa jana, alikuwa na msongo na mawazo na alishindwa kufanya shughuli zake vyema.

Alisema si yeye tu, hata familia yake haikuwa na raha kwa kuwa wakati wote walikuwa wanafikiria hatima yake dhidi ya tuhuma zilizokuwa zinamkabili.

"Ninamshukuru Mungu, Rais Mama Samia Suluhu Hassan na DPP kuona hana nia ya kuendelea na kesi hii na serikali kwa ujumla, sikuwa na raha, hata ndugu na familia yangu walikuwa kwenye wakati mgumu wakati wote tangu nishtakiwe, ninashukuru kuwa huru, ninakwenda kuendelea na ujenzi wa taifa wa awamu ya sita," alisema.

Katika kesi ya msingi, Lissu na wenzake walikuwa wanakabiliwa na mashtaka matano ikiwamo kuandika habari za uchochezi kinyume cha Sheria ya Magazeti ya Mwaka 2002.

Ilidaiwa kuwa kati ya Januari 12 hadi 14, 2016, jijini Dar es Salaam, washtakiwa Jabir, Mkina na Lissu, waliandika na kuchapisha taarifa za uchochezi zenye kichwa cha habari 'Machafuko yaja Zanzibar.'

Katika shtaka la pili wanadaiwa kuwa Januari 14, 2016 walichapisha habari hizo ili kuleta chuki kwa wananchi wa Zanzibar. Mshtakiwa Mehboob anadaiwa kuwa Januari 13, 2016 katika jengo la Jamana lililoko Manispaa ya Ilala, alichapisha gazeti la Mawio lililokuwa na taarifa za uchochezi. Ilidaiwa kuwa mshtakiwa huyo pia alichapisha gazeti hilo bila ya kuwasilisha hati ya sheria ya kiapo kwa Msajili wa Magazeti.

# Watanzania watahadharishwa magonjwa yasiyoambukiza

**Na Mwandishi Wetu**

IDADI ya watu wanaoathirika na magonjwa yasiyoambukiza (NCDS) inaongezeka duniani na kwa Tanzania asilimia 27 ya vifo vyote inasababishwa na magonjwa hayo.

Utafiti wa mwaka 2012 uliofanyika Tanzania ulionyesha kwa kila watu 100 wenye miaka 25 na kuendelea, tisa wana kisukari, 26 shinikizo la damu, 25 mafuta yaliyozidi kwenye damu na 34 wana uzito uliozidi.

Mwenyekiti wa Chama cha Kupambana na Magonjwa yasiyoambukiza nchini (TANCDA), Profesa Andrew Swai, aliwaambia wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari nchini kuwa kama Watanzania hawatabadili mienendo ya maisha, magonjwa hayo yatasababisha vifo vingi.

Alitaja baadhi ya vitu vinavyosababisha magonjwa hayo ni ulaji ovyo, chumvi, sukari na mafuta.

Alisema hayo wakati akielezea wiki ya uhamasishaji ya kupambana na magonjwa yasiyoambukiza inayotarajiwa kufanyika jijini Arusha kuanzia Oktoba 6 mpaka 13 yenye kaulimbiu ya 'Uhusishaji sekta mtambuzi katika kupambana na magonjwa yasiyoambukiza'.

Aliyataja baadhi ya magonjwa yasiyoambukiza kuwa ni moyo, shinikizo la damu, figo, sukari, magonjwa ya meno na kila mwaka watu milioni 15 duniani wanakufa kutokana na magonjwa hayo na wengi wanatoka katika nchi zinazoendelea. Akizungumzia athari ya magonjwa hayo, alisema kwa mwaka 1991, serikali ilitumia asilimia tisa ya bajeti yake kutibu wagonjwa wa kisukari.

Vile vile, alisema gharama zinazotumika katika sekta ya afya kwa mtu mmoja nchini Tanzania ni Dola za Marekani 37 kwa siku. Pato la ndani kwa mtu ni Dola 950.

Kuhusu namna ya kujikinga na magonjwa hayo, mtaalamu wa mazoezi kutoka Chama cha TANCDA, Waziri Ndonde, alisema watu lazima washughulikie miili yao dhidi ya tabiabwete.

Alisema ni muhimu kuzingatia kazi wanazozifanya kila siku, usafiri wanaotumia, michezo na mazoezi ambavyo vinamfanya mtu awe na utimilifu wa mwili.

Waziri alisema utimamu wa mwili ni uwiano unaohusisha viungo vya mwili visielemeane.

Alisema kufanya mazoezi kunamfanya mtu kuwa mkakamavu wa mwili na afya iliyo imara na kwamba kutokufanya mazoezi kunachukua nafasi ya nne ya vifo duniani. Kuhusu vyakula vinavyohitajika kupuka magonjwa hayo, Muuguzi Mwandimizi kutoka CDA, Elizabeth Licoco, alisema watu lazima wazingatie mlo kamili kila siku.

Alitaja vyakula vinavyotakiwa kuwa aina ya kwanza ni vyote vya mizizi, nafaka na ndizi. Aina ya pili ni maziwa, samaki, nyama, choroko, maharagwe (vinavyojenga mwili) na aina ya tatu ya mboga ambavyo hutoa nyuzinyuzi.

Nyingine ni matunda na mafuta, lakini yanayotokana na mbegu na yatumike kidogo.


# NOTISI / TANGAZO

**MUDU COMPANY LTD, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD, ,LEGENDS AUCTION MART LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,CHAMPION AUCTION MART,MAKI RECOVERIES LTD,PSALM AUCTION MART,MALAPA AUCTION MART,HEDANE ENTERPRISES LTD,KILICRAALS AUCTIONEER, DESTENI COMPANY LIMITED, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS,JY AUCTIONEERS CO.LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, BEST GROUP LTD, NGOMENI AUCTION MART,MOPEH COMPANY LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**, tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| CAROLINE ELISA SANGETI/ SEIA EBENEZA SCHOOL | SHULE NA NYUMBA | CAROLINE ELISA SANGETI & ELISA ISSACK SANGETI | KIJIJI CHA ENGORIKA KATA YA KISONGO | 07/10/2021 NA KUENDELEA |
| MY WAY INTERNATIONAL LTD/ALLEN ADAM SANGA | NYUMBA | ALLEN ADAM SANGA | UBUNGO-DAR ES SALAAM | 11/10/2021 NA KUENDELEA |
| STEVEN PIUS MALISA | NYUMBA | STEVEN PIUS MALISA | MTAA WA KITINYE-DAR ES SALAAM | 15/10/2021 NA KUENDELEA |
| BUMERA LOGDE AND CO LTD | NYUMBA | JOACHIM HERONIMUS MWINGIRA AND ASTERY MWITA NDEGE | MTAA WA KIGOGO KATI,KINONDONI – DAR ES SALAAM | 18/10/2021 NA KUENDELEA |
| MOHAMED ATHUMANI BAKARI | PAGALE-NYUMBA | MOHAMED ATHUMANI BAKARI | NDACHI KATA YA MNADANI-DODOMA | 07/10/2021 NA KUENDELEA |
| CLETUS CLAVERY KISAWIKE | PAGALE-NYUMBA | CLETUS CLAVERY KISAWIKE | MTAA WA MTUMBA – DODOMA | 08/10/2021 NA KUENDELEA |
| HEMEDI HARUNI RASHIDI | NYUMBA | HEMEDI HARUNI RASHIDI | KIJIJI CHA BAHI SOKONI – DODOMA | 09/10/2021 NA KUENDELEA |
| INOCENCIA JANUARY LUBINGA | NYUMBA | PETRO MASADU | MSISSI DODOMA | 11/10/2021 NA KUENDELEA |
| JANVIER VOSTER LUBINGA | NYUMBA | JANVIER VOSTER LUBINGA | MSISSI DODOMA | 12/10/2021 NA KUENDELEA |
| GEOFREY FEDRICK MHAKILICHA | NYUMBA | SHAIBU SOZI SALUMU | KATA YA MTUMBA – DODOMA | 13/10/2021 NA KUENDELEA |
| YESAYA SAMWEL KIBONDE | NYUMBA | YESAYA SAMWEL KIBONDE | SHEWA,MBEYA MJINI | 11/10/2021 NA KUENDELEA |
| LUSUBILO ANYAMBILIKE NGOBILE | GARI CANTER T607 BGE | LUSUBILO ANYAMBILIKE NGOBILE | ILOMBA,MBEYA MJINI | 09/10/2021 NA KUENDELEA |
| JEFTA NYASA MALULU | NYUMBA (3) | JEFTA NYASA MALULU | KANGAE 'A' MWANZA | 07/10/2021 NA KUENDELEA |
| MARTINA CORRONATUS RYOBA | KIWANJA NAMBA 562 KITALU "B" | MARTINA CORRONATUS RYOBA | BUJINGWA-MWANZA | 07/10/2021 NA KUENDELEA |
| WENCESLAUS JOHN MASSAWE | KIWANJA CHENYE NYUMBA AMBAYO HAIJA ISHA | WENCESLAUS JOHN MASSAWE & MATESO JOHN MASSAWE | MBWENI-KINONDONI | 7/10/2021 NA KUENDELEA |
| ESTER JEREMIA FOKAS | NYUMBA | ESTER JEREMIA FOKAS | KIVULE-ILALA | 29/10/2021 NA KUENDELEA |
| MUSSA NG'OMBE NKOBA | NYUMBA | ZUHURA ISSA FERUZI | MWONGOZO | 08/11/2021 N A KUENDELEA |
| YUSTER WESTON AYOLA | NYUMBA | SHABANI HARUNA MLENDA | MACHINJIONI, MBAGALA | 29/10/2021 NA KUENDELEA |
| MARIA GREGORY MKABAIRU | NYUMBA | ZAINA ALMASI BILALI | MSUMI-UBUNGO | 28/10/2021 NA KUENDELEA |
| SOPHIA MUSSA SELEMANI | NYUMBA YENYE HATI | SOPHIA MUSSA SELEMANI | MAGU-MWANZA | 08/10/2021 NA KUENDELEA |
| TIMOTHY LUCAS MANYAMA | NYUMBA | TIMOTHY LUCAS MANYAMA | KONGOWE-PWANI | 7/10/2021 NA KUENDELEA |
| ELIUD SIMON MHEMBU | NYUMBA | ELIUD SIMON MHEMBU | GOBA | 7/10/2021 NA KUENDELEA |
| JOHNSON ELIEZA MUKIZA | NYUMBA | JOHNSON ELIEZA MUKIZA | KWEMBE-UBUNGO | 7/10/2021 NA KUENDELEA |
| MDAKI NASSORO KABELELE | NYUMBA | MDAKI NASSORO KABELELE | MAJOHE | 12/10/2021 NA KUENDELEA |
| BOSCO THADEI UTENGA | NYUMBA | BOSCO THADEI UTENGA | KIGEZI-ILALA | 7/10/2021 NA KUENDELEA |
| WANSAGULA MOSES NATUMWA | NYUMBA | PILI HARUNA BUHANGWA | PUGU-ILALA | 7/10/2021 NA KUENDELEA |
| ABDULRAHMAN RAJAB MAHABA | NYUMBA | ABDULRAHMAN RAJAB MAHABA | ZINGIZIWA-ILALA | 8/10/2021 NA KUENDELEA |
| NASHON RANGE ROTENTE | NYUMBA--2 | NASHON RANGE ROTENTE | PUGU NA MBONDOLE | 8/10/2021 NA KUENDELEA |
| LAURENT ERNEST MADEGE | NYUMBA | LAURENT ERNEST MADEGE | VINGUNGUTI-DSM | 7/10/2021 NA KUENDELEA |
| ABUKA COMPANY LIMITED | NYUMBA | ALILIUS BUTEMBERO ADOLPH | BOKO-KINONDONI | 11/10/2021 NA KUENDELEA |
| AUGUSTINO KILUNDE SANGA | NYUMBA | AUGUSTINO KILUNDE SANGA | TANDALE | 12/10/2021 NA KUENDELEA |
| JOHANES MARWA RYOBA | NYUMBA | JOHANES MARWA RYOBA | MAVURUNZA | 13/10/2021 NA KUENDELEA |
| SABRINA SALMIN RAJABU | NYUMBA | SAIDI RAMADHANI MAGONA/ZAINA ABDALLAH JUMA | MAKURUMULA | 13/10/2021 NA KUENDELEA |
| UPENDO SIMON MEDADI | NYUMBA | JOHN OBADIA MORIS | BUNJU | 14/10/2021 NA KUENDELEA |
| ZAINABU LUPA SUDI | NYUMBA | RAJABU MTORO RAJABU NA ZAINABU LUPA SUDI | KINGUGI KWAZOMBOKO | 07/10/2021 NA KUENDELEA |
| MONICA AIDAN KIHAMPA | NYUMBA | KALEBU ZAKARIA MAGEMBE | MPONDA | 08/10/2021 NA KUENDELEA |
| GESINE GESINE MWITHABE | NYUMBA | ROSE ALEX KIMARO | MBAGALA SABASABA BUGUDADI | 09/10/2021 NA KUENDELEA |
| EDINA MOSES MTEI | NYUMBA | DONATH JOHN KALEBU/RONATHA J MWANGOSI | MTONI KIJICHI | 11/10/2021 NA KUENDELEA |
| MECKSON KAGOMA MSANZE | NYUMBA | MECKSON KAGOMA MSANZE | MPONDA | 12/10/2021 NA KUENDELEA |
| GRACE ANTONY MGATA | NYUMBA | GRACE ANTONY MGATA | YANGEYANGE MSONGOLA | 13/10/2021 NA KUENDELEA |
| MARIAM MOHAMED LUKWAYO | NYUMBA | MARIAM NA MATATIZO CHEMBERA | VIANZI | 14/10/2021 NA KUENDELEA |
| PAULO JACOB MUHAMARY | NYUMBA | HASSAN MOHAMED TINDWA | KIMANZI CHANA | 15/10/2021 NA KUENDELEA |
| OTHMAN SHAIBU MILANZI | NYUMBA | OTHMAN SHAIBU MILANZI | TUNDWI SONGANI TEMEKE | 18/10/2021 NA KUENDELEA |
| TAUSI SUBIRI KIBAIZI | NYUMBA | MR & MRS TAUSI WENCHENSLAUS | MSONGOLA | 20/10/2021 NA KUENDELEA |
| SUZAN PETRO KOMUGISHA | NYUMBA | SUZAN PETRO KOMUGISHA | VIKINDU | 29/10/2021 NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwamnunuziatashindwakutimizashartilolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwapesayoyotealiyokwishailipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. 0754497396 / 0713077474 / 0689349477 / 0768672367 / 0714939933 / 0718038313 / 0715363537 / 0784252048
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

216471601

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wamachinga waendelezwe kwa kuwainua huko waliko

**SERIKALI** imetangaza mpango wa kuunda idara mahusus ya kushughulikia viwanda, biashara na uwekezaji kwa kila halmashauri pamoja na kuanzisha dawati litakalotatua kero za wamachinga.

Hatua hiyo ni kutekeleza maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, ya kuwapanga upya wafanyabiashara hao na kwamba utekelezaji umeanza kwa kufufua idara ya uendelezaji miji na vijiji, ili maofisa mipango miji na vijiji watime kazi zao kiufanisi.

Hatua hiyo, inatangazwa wakati wa kuzindua mpango wa kuwapanga wamachinga kwenye vibanda 652 katika Soko Kuu la Chifu Kingalu, Manispaa ya Morogoro vilivyogharimu Shilingi milioni 81.7.

Aidha, ni maagizo ya serikali kila halmashauri itenge maeneo maalum kwa ajili ya wafanyabiashara hao, ambayo pia yataendelezwa ili kuzuia wimbi la vijana kutoka vijijini kuhamia mijini.

Tunaunga mkono utaratibu wa kuwapanga machinga kwenye miji yetu, ili kuondoa usumbufu wanaopata watumiaji wengine wa barabara na maeneo mengine ya biashara.

Wamachinga wamekuwa kero, wamejaa kwenye vituo vya mabasi, ndani ya barabara na hifadhi zake, wapo kwenye madaraja na njia za wanaotembea na wengine wamevamia baraza na viambaza vya maduka kwenye maeneo ya biashara bila kujali.

Yote hiyo ni kwavile idadi ya vijana wanaotoka vijijini kukimbilia mijini ni kubwa mno kutokana na ukosefu wa miundombinu ya kuendeleza 'kusapoti' biashara zao. Ni ukweli kuwa maendeleo vijijini si makubwa, hakuna huduma za jamii kama barabara, umeme, wala miundombinu ya kufanikisha biashara zao, lakini mzunguko wa fedha ni mdogo hivyo suluhisho jepesi ni vijana kuondoka.

Serikali inathibitisha kuwa idadi ya wanaotoka vijijini kwenda mjini ni kubwa, hivyo tunaona kuwa kuna haja ya kupata suluhisho la kupunguza idadi ya wanaokimbilia mijini.

Hii itawezekana iwapo serikali itawaandalia mazingira ya kuwekeza sehemu walizopo na siyo vingine, mathalani kuona namna bora ya kuzitumia barabara kuu kutoka mikoani kwenda kwenye majiji kuweka vituo vikuu vya kibiashara.

Kila halmashauri za miji na majini kuweka maeneo maalumu ya kibiashara yanayowawezesha wakulima, wafugaji, wavuvi, wasukaji na wachongaji kuuza bidhaa zao kupitia vituo hivyo.

Iwapo vitaboreshwa na kuuza bidhaa zinazozalishwa vijijini na kwenye maeneo yao ni dhahiri wafanyabiashara kutoka miji mikubwa na majiji watasafiri kuwafuata wamachinga huko waliko na kununua bidhaa zao. Ni wazi kuwa wamachinga wengi mijini wanauza bidhaa kutoka nje ya nchi kama mavazi (nguo, viatu, mikoba vya mitumba), wapo wanaouza vyombo, toi na kundi jingine vyakula kuanzia matunda, mboga hadi vilivyopikwa kama chips na nyama, ambavyo si endelevu.

Tunaona kuwa ni muhimu kuweka mkazo kwenye kuendeleza miji, vijiji na maeneo mbalimbali kwa kuvipelekea umeme, maji, barabara, viwanda, makazi ya kisasa, masoko, minada na vituo vya biashara ili wananchi vijana wapende kubaki kwenye maeneo yao badala ya kukimbilia mijini na majijini.

Tunashauri kuwa huo utakuwa ufumbuzi muhimu kwavile tumekuwa tukiwajengea vizimba mijini na kuwagawia, hicho kimekuwa kichocheo cha kuwavuta wenzao kuhamia kwa wingi.

Tunapendekeza walioko mijini na majijini kwenye vizimba kuwe na ufuatiliaji kujua wafanyabiashara hawa wanakua kibiashara au miaka yote wanabaki kuwa machinga kwa kuwa kuna mteremko hasa kwavile hawana wasiwasi na kodi ya pango kwasababu pango kizimba au mikono yao.

Lakini tusiishie hapo serikali ikomeshe ujanja wa kuwatumia kuuza bidhaa ili kukwepa kodi kunakofanywa na wafanyabiashara wakubwa ili mpango huo wa kuwaendeleza uwe na tija.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Pongezi Rais Samia, namna ulivyoingilia kati ya Machinga



Na Ester Mgidula

**MOJA** ya tabia kubwa ambayo binadamu tunayo, ni kwamba kuna wakati huwa ni wepesi wa kupuuza baadhi ya mambo. Lakini, yakishakuwa makubwa au mazito, ndipo hapo tunaanza kujiuliza nini kilitokea.

Kupuuza ni hulka ya asili ambayo kila mwanadamu anayo kwa viwango tofauti na ndiyo maana, huwa kuna msemo unaoeleza kiongozi mzuri ni yule anatatua matatizo ya watu wake, lakini kiongozi bora ni yule ambaye anaona tatizo kabla halijatokea.

Mara nyingi dhana hiyo ya kutatua tatizo, ndiyo ambayo huwa inachukuliwa na wengi kwa mtazamo wa mkumbo kuwa ndiye kiongozi bora, lakini kiuhalisia yule ambaye anaona tatizo kabla halijatokea, ndiye anayestahili kupewa pongezi mama analishinda tatizo.

Kwanini nasema hivyo? Mara nyingi hasa kwenye hizi sekta kubwa au nafasi kubwa, viongozi wengi wanapenda kuwa katika upande wa wale wanaotatua matatizo kwa kuwa wanajua watapata sifa nyingi na wataonekana ndiyo wanaostahili.

Wale ambao wanatatua matatizo kabla hayajatokea huo ndiyo wa muhimu zaidi, lakini kwa kuwa tu jamii ya watu haiwaoni au haioni kile kinachofanywa na wao, basi umuhimu wao unaonekana mdogo.

Kwa sasa, kuna sakata la Wamachinga na jinsi ya kuweka utaratibu mzuri wa wao kufanya biashara. Tofauti na ilivyo sasa, asilimia kubwa wanafanya kiholela bila ya kuwa na mpangilio sahihi.

Wamachinga licha ya kuwa ni ndugu zetu, familia, marafiki na jamaa zetu, lakini ukweli ni kuwa kuna tatizo kubwa linatokana na wao kukosa utaratibu mzuri wa kufanya shughuli zao.

Suala hilo lilitakiwa kuwa limeshafanyia kazi miaka mingi nyuma ja ka ya kukua kufikia hatua ya sasa. Tatizo hilo nalo limekuwa likiendelea kila mwaka.

Ni kweli wamachinga wanahitaji kufanya biashara zao, lakini kila kiongozi anapoingilia kutaka kufanya au kuweka utaratibu mzuri wa kuwawezesha waendelee na biashara zao, bila ya kuwavuruga watu wengine. Inakuwa ngumu kuwa tayari kwa sababu nguvu ya wamachinga iko kubwa.

Kwa maisha ya Kitanzania yalivyo sasa, ni lazima kila Mtanzania awe anajihusisha kwa namna moja au nyingine katika biashara hii, iwe kwa mtu wake anashiriki kuuza au yeye mwenyewe kutegemea kununua bidhaa kutoka kwa machinga.

Kwa msingi huo, inamaanisha kuwa sakata la wamachinga ni mzizi mkubwa ambao kuudhibiti unahitaji akili kubwa. Kutumia nguvu pekee, ni kuingia katika matatizo makubwa.

Nampongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuligusia suala hilo la wamachinga. Anajua wazi kuingia kutumia nguvu pekee haitasaidia, ndiyo maana ameagiza utumike utaratibu wa mazungumzo na kueleweshana.

Kwa kawaida, kunaelezwa kuwapo baadhi ya wafanyabiashara wakubwa wamekuwa wakilazimika kutumia wamachinga katika kuuza biadhaa zao.

Niseme, kufanya hivyo kunamaanisha kuwa suala la kodi ni mtihani, serikali inakosa chake cha kuisaidia kuendesha nchi.

Kama tabia hiyo, itaendelea kuachwa na itafika hatua itaonekana ni kawaida, huku serikali iikipoteza fedha nyingi kutokana kusuasua katika kuchukua uamuzi mapema.

Nirejee maelezo ya Rais Samia ni ya msingi sana. Anatambua kuwa suala la wamachinga kwa sasa hutakiwi kuliingilia 'kichwa kichwa', kwani kufanya hivyo ni kutengeneza mazingira ya kukosekana kwa imani hasa kwa maeneo mengi.

Machinga wanaendesha maisha yao na familia zao katika sura oana inayofika mbali. Idadi yao ni mamilioni ya watu, hivyo kuwaondoa ghafla kwenye utaratibu wao, inamaanisha kuwa ni kuwatengeneza matatizo mengine.

Licha ya kwamba natambua nguvu ya serikali ni kubwa na inaweza kufanya au kuamua chochote kikubwa na wamachinga wakatakiwa kutii, lakini alichokifanya Rais Samia ni kuona tatizo kabla halijatokea.

Pia, mara zote binadamu unapomshirikisha katika kutua tatizo lake, ni rahisi sana kupata ufumbuzi ambao ni bora.

Muhimu ni kuwa hata wale viongozi wa mikoa na ngazi nyingine waliopewa maagizo na Rais kuhakikisha suala la wamachinga ninarejea katika mstari mzuri, wanatakiwa kufanya kwa usahii, tofauti na hapo watamtengenezea bomu kiongozi wetu na baadaye lije lilipuke.

# Mahakama ya rufani yabariki miaka 30 jela

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Rufani Kanda ya Mbeya imebariki Ombeni Sanga kutumikia kifungo cha miaka 30 jela kwa kumwingilia kinyume cha maumbile binti yake mwenye umri wa miaka 12.

Uamuzi huo umefikiwa na jopo la majaji watatu, Jaji Dk. Gerald Ndika, Jaji Barke Sahel na Jaji Penterine Kente baada ya kupitia sababu za kupinga adhabu aliyopewa mahakama za chini mkoani Mbeya.

Ombeni alishtakiwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya akidaiwa Oktoba 12, 2016, maeneo ya Itezi, Iyunga mkoani Mbeya, alimwingilia kinyume cha maumbile binti yake wakati huo akiwa na miaka 12.

Katika kesi hiyo, Jamhuri iliita mashahidi watano na kielelezo kimoja ambacho ni ripoti ya daktari ili kuthibitisha kosa dhidi ya mlalamikaji.

Inadaiwa katika ushahidi kwamba mlalamikaji ni baba wa binti, alikuwa akiishi naye na siku ya tukio alimwambia mtoto abaki nyumbani, akaenda kukata nyasi kwa ajili ya kulisha ng'ombe.

Mlalamikaji aliporudi nyumbani binti alikuwa amekwenda kucheza na watoto wenzake, baba alimtafuta na alipompata alimtisha kwamba atamjua yeye nani.

Inadaiwa alienda kukata fimbo kwa lengo la kumchapa, alimfuata chumbani na kumtaka achague kimoja wapo kati ya vitu viwili alivyomwambia.

Alitaka achague amwingilie kinyume na maumbile au amruhusu ambake lakini mtoto alikaa kimya kisha alianza kulia.

Inadaiwa katika ushahidi kwamba, Ombeni alichukua blanketi na kumfunika usoni mwanawe kisha alimwingilia na baada ya kumaliza alitoka nje kulisha ng'ombe wake. Binti alipoona baba yake ametoka alipata nafasi ya kukimbilia kwa jirani ambaye ni shahidi wa tatu katika kesi hiyo, akasimulia alichofanyiwa.

Inadaiwa alirudi nyumbani akiwa na jirani pamoja na mjumbe wa nyumba kumi, baba alikamatwa na kupelekwa polisi.

Baada ya ushahidi huo, Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya ilimtia hatiani na kumhukumu kifungo cha miaka 30 jela.

Mlalamikaji alipinga adhabu hiyo Mahakama Kuu Mbeya lakini alishindwa na kukimbilia Mahakama ya Rufani ambayo pia imetupilia mbali rufani yake.

Alitoa sababu mbalimbali za kupinga adhabu ikiwamo Mahakama Kuu ilikosea kisheria kutupa rufani yake kwa kuegemea katika ushahidi wa binti na ilikosea baada ya kupokea ripoti ya daktari kama kielelezo hakikusomwa na utetezi wake haukuzingatiwa.

Jopo la majaji baada ya kupitia hoja zilizowasilishwa na mlalakaji na majibu ya upande wa Jamhuri, liliona ushahidi wa mtoto uwe umechukiliwa peke yake ama pamoja na ushahidi wa shahidi wa pili, unatosha kusapoti adhabu aliyopewa mlalamikaji.

"Utetezi wa mlalamikaji ulizingatiwa kama inavyoonyesha katika kumbukumbu za mahakama na mahakama inatupilia mbali hoja kwamba wakati tukio hilo linatokea mlalamikaji hakuwa nyumbani," ilisema sehemu ya hukumu hiyo.

Mahakama ilitupilia mbali rufani baada ya kukubaliana na uamuzi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya, Mahakama Kuu Mbeya kwamba Jamhuri ilithibitisha mashtaka bila kuacha shaka.

Rufani ilitupwa na mrufani anaendelea kutumikia kifungo cha miaka 30 jela.

# NMB sasa yajitosa kufufua sekta utalii

**Mwandishi Wetu, ARUSHA**

BENKI ya NMB imewahakikishia wawekezaji katika sekta ya utalii kuwa ipo tayari kushirikiana nao kufufua na kuendeleza sekta hiyo iliyoathirika vibaya na janga la virusi vya Covid-19 ambalo limeathiri sekta ya utalii ulimwenguni.

Mkuu wa Idara ya Biashara ya NMB, Alex Mgeni alisema hayo wakati wa maonyesho ya utalii ya Tanzania Tourism Summit yaliyofanyika jijini Arusha, ambayo benki hiyo ilikuwa mdhamini mkuu.

Alisema sekta ya utalii inategemea watu kusafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine, lakini baada ya janga la ugonjwa wa corona kulikumba dunia nchi mbalimbali ziliweka vikwazo vya usafiri ili kuthibiti kusambaa zaidi kwa ugonjwa huo.

"Benki yetu inatambua changamoto kubwa ambayo mmepitia wadau wa sekta ya utalii, tuna taarifa za wafanyakazi kupoteza ajira kwenye mahoteli ya kitalii mbugani,makambi ya kudumu na yale ya muda pamoja wafanyakazi wa kada zingine, NMB imejipanga kuingilia kati kuona utalii unarudi kwa kasi," alisema Mgeni.

Katika kuthibitisha utayari wa benki hiyo kuwawezesha mikopo wawekezaji wa sekta ya utalii, alisema mteja anaweza kujipatia hadi kiasi cha Sh. bilioni 5 kwa mkupuo ambao atautumia kupanua wigo wa uwekezaji wake utakaochangia kutoa huduma za hali ya juu kwa watalii na kuongeza ajira.

Awali Meneja wa NMB Kanda ya Kaskazini, Dismas Prosper, alisema benki hiyo inatambua sekta ya utalii kuwa mojawapo ya maeneo wanayoyapa kipaumbele kwasababu yanachangia biashara ya fedha za kigeni.

"Mikoa ya kanda ya Kaskazini hasa Arusha, Kilimanjaro na Tanga inategemea sekta ya utalii kwa kiwango kikubwa milango yetu ipo wazi kuwasikiliza na kuhakikisha hampati kikwazo chochote cha kifedha kuiendeleza sekta hii inayoweza kutoa mchango muhimu kwa uchumi wa nchi yetu," alisema Dismas.

Mkurugenzi wa taasisi ya Tanzania Tourism Summit iliyoandaa maonesho hayo, Tom Kunkler, alisema benki hiyo imekuwa mshirika mwaminifu katika kudhamini maonyesho yanayochochea kukuza sekta ya utalii nchini na kuahidi kuendelea kushirikiana nao.




LAWS OF LOVE IS A TELENOVELA ABOUT PROFESSIONAL LAWYERS WORKING FOR A LEGAL FIRM CALLED VEGA. THE STORY EVOLVES AROUND LOVE, JEALOUSY, GREED, HATRED AND BETRAY WHEN THE LAWYERS MIX LOVE WITH PROFESSIONAL WORK.

DON'T MISS THIS CAPTIVATING TELENOVELA, STARTING ON 5TH OCT 2021 CAPITAL TELEVISION.



TAJIRI NA BILIONEA LEON CARVAHAL AJIKUTA MLENGWA WA WABAYA WAKE, AMALIZWA KIKATILI SIKU YA HARUSI YAKE, ROHO YAKE YAJITOKEZA UPYA KWA CHINO VALDES KIJANA MTUKUTU NA MHALIFU ANAYEOGOPEKA AMBAYE NAYE ALIMALIZWA KWA HUKUMU YA KITI CHA UMEME. NA MWISHO PROFESA BETRAN CAMACHO NAE APATA AJALI MBAYA YA GARI NA KUFARIKI DUNIA.
HAWA WOTE WATATU WAFARIKI MUDA MMOJA, MAENEO, VYANZO NA MAZINGIRA YA VIFO VYAO NI TOFAUTI.
JE, NI NANI WAHUSIKA WA VIFO HIVI VITATU?.

LOVE TO DEATH KUANZIA TAREHE 4 OKTOBA SAA 4:10 USIKU ITV PEKEE!!

ITV

# Wizara yasisitiza marufuku hospitali kuzuia maiti

**Na Mary Geofrey**

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imesema inatekeleza maagizo yake kuhusu marufuku kwa hospitali zote nchini kuzuia maiti kwa sababu ya ndugu kushindwa kulipa deni la mgonjwa.

Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifelo Sichwale, alilieleza Nipashe jana kuwa, utekelezaji wa maagizo ya wizara hiyo, yanasimamiwa chini ya kanuni na taratibu za leseni za kuendesha hospitali na vituo vya afya na siyo vinginevyo.

"Maelekezo ya serikali yapo wazi mbona, kuwa mgonjwa anapoenda kutibiwa ikatokea bahati mbaya akafariki maiti hakuna kuzuiliwa, ndugu wapewe mwili na hayo mambo mengine yaendelee baadaye," alisisitiza Dk. Sichwale.

Kuali hiyo anaitoa ikiwa ni siku moja baada ya kuibuka kwa matukio mawili tofauti ya miili ya watu waliofariki dunia kuzuiliwa. Ikiwamo Hospitali ya Taifa Muhimbili inayodaiwa kuzuia mwili kutokana na ndugu kushindwa kulipa deni la Sh. milioni 1.5 ikiwa ni gharama za matibabu ya mgonjwa.

Tukio lingine limetokea katika hospitali moja ya mkoani Dar es Salaam (jina tunahifadhi) inadaiwa walizuia maiti kwa sababu ya kutaka ndugu walipe gharama za matibabu ya mgonjwa wao Sh. milioni mbili.

"Kuhusu suala la Muhimbili leo (jana) wanatoa maelezo kuhusiana na tukio hilo na kuhusu hiyo hospitali (aliitaja jina), sijafahamu sababu za kuzuia mwili wa marehemu ni nini," alisema Dk. Sichwale.

Alisema kuwa maelekezo, miongozo na taratibu tunawapa wenye hospitali au kituo cha kutolewa huduma za afya, hivyo ikitokea taratibu zinakiukwa inatakiwa ifahamike tatizo liko wapi.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa MNH, Aminiel Aligaesha, akifafanua suala hilo, alisema ndugu wa marehemu alitakuwa kulipa deni hilo, lakini hakurudi kwa uongozi kusema ameshindwa kulipa na badala yake alikimbilia kwenye vyombo vya habari.

Matukio hayo yanatokea ikiwa ni siku chache tangu Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam, Amos Makalla, kupiga marufuku hospitali kuzuia miili ya marehemu kwa sababu mgonjwa kushindwa kulipa fedha za matibabu na badala yake, mwili ukabidhiwe kwa ndugu wa marehemu kwa ajili ya maziko wakati taratibu nyingine zinaendelea.

Makalla alitoa maelekezo hayo baada ya kupokea malalamiko ya wananchi kuhusu baadhi ya hospitali mkoani humo kuendelea na utaratibu wa kuzuia maiti licha ya serikali kupitia Wizara ya Afya kukataza uzuiaji wa maiti.

Aliwaelekeza waganga wakuu wa wilaya chini ya wakuu wa wilaya kuhakikisha tatizo hilo halijirudii katika maeneo yao.

Juzi gazeti moja liliripoti Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), kuzuia maiti kwa sababu ndugu walishindwa kulipa gharama za matibabu.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa, maiti ya Zena Mussa Ramadhani (30) ilizuiliwa kutokana na deni la Sh. milioni 1.6 waliyokuwa wakidaiwa ndugu kutokana na matibabu aliyopatiwa ndugu yao hospitalini hapo.

Mwishoni mwa mwaka jana, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, aliagiza lutozuiliwa kwa miili ya marehemu na kuzitaka hospitali kuwakabidhi ndugu pindi wanapohitaji kufanya hivyo.

Aidha, alizitaka hospitali zote kuhakikisha zinatambua mapema na kuwasiliana na ndugu wa mgonjwa wanapoona inashindikana kulipia gharama za matibabu kwa wakati ili mgonjwa atibiwe kwa msamaha.

Itakumbukwa pia Februari 14, mwaka jana, aliyekuwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alipiga marufuku hospitali kuzuia miili ya marehemu kwa sababu ya madeni.



Mtaalamu wa hesabu, Wesley Nsomba, akiwasilisha mada kuhusu usimamizi wa fedha kwenye miradi ya ujenzi wakati wa mafunzo ya siku tatu kwa makandarasi wazalendo yanayoendelea jijini Mwanza kwa uratibu wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi nchini (CRB). **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# 'Makandarasi wanatozwa faini na riba kubwa TRA'

**Na Joseph Mwendapole,**

MWANZA

IMEELEZWA kuwa makandarasi wengi wamekuwa wakitozwa faini na riba kubwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kutokana na kukosa uelewa wa masuala ya kodi na usimamizi wa fedha kwenye kampuni zao.

Hayo yalisemwa jana jijini Mwanza na mtaalamu wa masuala ya fedha, Wesley Nsomba, wakati akiwasilisha mada kuhusu usimamizi wa fedha na ukaguzi wa mapato na kodi kwenye kampuni za ujenzi.

Mafunzo hayo yaliyoandaliwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), yanawashirikisha makandarasi kutoka mikoa mbalimbali kwa ajili ya kuwajengea uwezo kuhusu usimamizi wa fedha, kodi na usimamizi wa mitaji.

Alisema makandarasi wote wanapaswa kujua masuala ya fedha, sheria zinazosimamia masuala ya kodi, ili kuepuka penati na riba zinazoumiza kampuni zao.

Nsomba alisema kampuni nyingi za makandarasi zinashindwa kulipa washauri mahiri wa kodi hivyo kujikuta wakishindwa kutimiza matakwa ya sheria na kuishia kutozwa kodi wakati mwingine kubwa kuliko uhalisia.

"Wenye kampuni za ujenzi wanapaswa kujua vyema usimamizi wa fedha na kodi kwa sababu TRA wanapowakagua vitu vingi wanakuwa hawajui sasa ndiyo maana CRB inawapa mafunzo ili wasiingie kwenye matatizo kama hayo," alisema Nsomba.

Aliwataka makandarasi hao kuhakisha wanakaguliwa hesabu zao kwa kuwatumia wataalamu wa fani hizo wanaotambuliwa na TRA kwani iwapo mamlaka hiyo inapokuja kuzikagua wanaingia kwenye matatizo ya kulipa kodi wakati mwingine kubwa kuliko uhalisia.

"Na mkiweka mshauri wa kodi hakikisheni mnakuwa na mkataba naye ili akiharibu mpate mwanya wa kumbana, msifanye naye kazi kiujanja ujanja kwasababu mwisho wa siku mambo yanapokuwa magumu TRA yeye anaweza kuwakana," alisema.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Riziki Kyoba, alikiri kuwa kampuni nyingi za makandarasi wazalendo zimekuwa zikiingia kwenye matatizo linapokuja suala la ukaguzi wa mahesabu kutokana na kuwatumia washauri wa hesabu vishoka.

Alisema mara kadhaa washauri hao wanapobanwa na TRA wamekuwa wakiwaita wenye kampuni kwenda kuchuana kwenye masuala ya sheria za kodi na maofisa wa mamlaka hiyo.

"Wewe unampa kazi mshauri wa kodi ambaye unatarajia ndiye akusaidie kujibu maswali TRA akibanwa anakwambia unaitwa TRA, hii si sahihi kwani ni sawa na kufuga mbwa halafu unabweka mwenyewe," alisema.

# Jiji Dar kuyakopesha makundi maalum bil. 1/-

**Na Mwandishi Wetu**

HALMASHAURI ya Jiji la Dar es Salaam imeidhinisha zaidi ya Sh. bilioni moja kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Ofisa Maendeleo ya Vijana wa halmashauri hiyo, Happiness Joachim, wakati akifungua mafunzo kwa vijana ya uwekezaji na elimu ya msingi ya fedha yaliyoandaliwa na Shirika lisilo la Kiserikali la CAFLO chini ya ufadhili wa Shirika la Foundation for Civili Society (FCS).

Alisema fedha hizo zimeidhinishwa katika mwaka mpya wa fedha 2021/22, vikundi vyote vitakavyostahili kupewa mikopo hiyo vitakopeshwa na kutakiwa kurudisha marejesho kwa wakati.

Alisema licha ya kupokea maombi mengi ya mikopo kutoka kwa vijana, halmashauri hiyo imeandaa utaratibu mzuri utakaohakikisha kila mwombaji ananufaika.

"Ni kweli sasa hivi utoaji wa mikopo unachukua muda mrefu kidogo kwa sababu mifumo imebadilishwa ikiwamo utaratibu wa ukusanyaji fedha, lakini utoaji wa mikopo unategemea na fungu tunalolipa na ndio maana kwa robo ya kwanza ya mwaka mpya wa fedha tayari kiasi za zaidi ya bilioni moja kimeshaidhinishwa na kitatolewa kwa walengwa," alisema.

Naye mwezeshaji katika mafunzo hayo kwenye mada ya ujasiriamali, William Mbuguma, alisema vijana watakaobahatika kupata mikopo hiyo wahakikishe wanaanzisha miradi itakayowaingizia kipato na kuwakwamua kiuchumi.

"Mara zote tumekuwa tukiwasisitizia vijana hawa wawe wajasiriamali na pindi wanapofanikiwa kupata mikopo hiyo waitumie kwa malengo iliyokusudiwa na si vinginevyo," alisema.

Mratibu wa miradi kutoka CAFLO, Emmanuel Ngazi, alisema moja ya malengo ya mafunzo hayo ni kuimarisha na kuendeleza vikundi au majukwaa ya vijana kwa kuwawezesha kupata elimu na mbinu za kuwekeza katika shughuli zinazowawezesha kukuza uchumi.

# Watoto yatima miaka mitano watumikishwa kazi mbaya

**Na Rehema Mbinda,** TUDARCo

ROBO ya watoto yatima milioni 3.2 wenye miaka mitano hadi 14, wanafanyakazi za kutumikishwa kinyume cha sheria ya mtoto.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa na Ubalozi wa Marekani nchini, serikali ya Marekani inasherehekea miaka mitano ya kutunza watoto yatima, walio kwenye mazingira hatarishi na kuwawezesha vijana kupitia mradi wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa wa Kizazi kipya.

Taarifa hiyo ilieleza: "Familia ni nguzo ya msingi katika kuwalinda watoto, lakini umaskini na magonjwa vinapunguza uwezo wa familia kuwahudumia watoto kikamilifu. Matokeo yake watoto wengi hususani walio chini ya miaka mitano wanakumbwa na magonjwa yanayoweza kuzuilika, udumavu na kuchelewa katika hatua za makuzi ya awali."

Katika mkutano uliofanyika jijini Dar es Salaam, pamoja na mengine ulijadili mafanikio na hatua itakayofuata katika kuhudumia watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi na kuwawezesha vijana kupitia mradi huo.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), Kate Somvongsiri, alisema: "Watoto wanapokuwa na afya na ustawi bora, elimu na wakipata usaidizi kutoka kwa walezi na jamii zao, watakuwa na msingi na mbinu bora za kuwa vijana wazalishaji na kuwa katika nafasi nzuri ya kufikia malengo yao. Hiki ndio kipaumbele kwa serikali zote mbili, serikali ya Tanzania na serikali ya Marekani."

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, kwa miaka mitano umetumia kiasi cha Dola za Marekani milioni 163.3 kuwawezesha watoto yatima, vijana wanaoishi na maambukizi pamoja na walezi wao kupata huduma stahiki zinazohusiana na Ukimwi kwa kuzingatia umri wao ili kuboresha hali zao za afya, lishe, elimu, ulinzi na usalama wa mtoto, ustawi wa maisha na ustawi wa kisaikolojia.

"Mradi uliamsha ari ya kutafuta huduma za Ukimwi, kupunguza vikwazo vya upatikanaji na utumiaji wa huduma za VVU na Ukimwi, na ufuatiliaji wa karibu kwa idadi ya watu waishio na virusi vya Ukimwi wanaositisha matumizi ya dawa," ilisema taarifa hiyo na kuongeza:

"Kwa muda wa miaka mitano iliyopita Kizazi Kipya ilifanya kazi kwa ukaribu na serikali ya Tanzania na Asasi zisizo za kiserikali kuwahudumia watoto yatima milioni 1.2 na takribani walezi 470,000 ili kuhakikisha kuwa vijana hawa wanapata huduma zinazohusiana na VVU na Ukimwi kulingana na umri wao na kupatiwa huduma ili kuboresha hali za maisha yao."

Taarifa hiyo ilisema kuwa zaidi ya vikundi vya kuweka na kukopa 12,200 vijulikanavyo kama WORTH Yetu viliundwa, na kwamba vimekusanya zaidi ya Sh. bilioni 26.6.



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko (wa pili kulia), akikabidhi mitungi ya Oksijeni 10, kwa Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga, Dk. Richard Mhangwa, iliyotolewa na kikundi cha Whatsapp cha "Okoa Uhai Nunua Mitungi", wilayani humo jana, kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma kwa wagonjwa wenye tatizo la UVIKO-19. Kulia ni Mratibu wa kikundi hicho, Gwakisa Mwasyeba. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Hospitali yapigwa jeki mitungi ya oksijeni

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

HOSPITALI ya Rufani mkoani Shinyanga, imepewa msaada wa mitungi 10 ya hewa ya oksijeni, kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma kwa wagonjwa, ambao wanakabiliwa na changamoto ya upumuaji.

Msaada huo ulitolewa jana na kikundi cha Watsap Mjini Shinyanga kiitwacho Okoa Uhai nunua mitungi, kilichoanzishwa kwa ajili ya kuchangisha kununua mitungi ya hewa ya oksijeni, ili kuokoa maisha ya wagonjwa wenye changamoto ya upumuaji wakiwamo wa UVIKO -9.

Mratibu wa kikundi hicho, Gwakisa Mwasyeba, alisema alianzisha kikundi hicho kwa lengo la kuhamasisha wadau mbalimbali kuchangishana fedha na kununua mitungi ya hewa ya oksijeni, ili kuokoa uhai kwa wagonjwa wenye matatizo ya upumuaji, ambao wanapatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, alisema ni jambo la heli kuona wadau wanaendelea kusaidiana na serikali, kuboresha utoaji wa huduma kwa wagonjwa wenye matatizo ya upumuaji.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga, Dk. Richard Mhangwa, alisema msaada wa mitungi hiyo utaongeza idadi ya mitungi iliyopo na kumaliza kabisa tatizo la upungufu wa mitungi na kuboresha utoaji wa huduma.

# ACB yaona mafanikio huduma Akiba Wakala

**Na Enock Charles**

BENKI ya Biashara ya AKIBA (ACB) imesema imeona nuru ya mafanikio kutoka kwa wateja wake kupitia huduma yake ya Akiba Wakala, ambayo imetimiza mwezi mmoja tangu iingie sokoni.

Mafanikio yaliyopatikana yanakuja wakati ACB inatarajia kufikia angalau wateja wa 100,000 na wasio wateja katika miezi mitatu ijayo kupitia huduma hiyo.

Dora Saria, Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano wa benki hiyo, alisema kuwa ndani ya mwezi mmoja tangu huduma hiyo ianzishwe sokoni, imevutia maelfu ya watumiaji.

"Tunatarajia kuwafikia wateja zaidi ya 100,000 wa Akiba Wakala kwa wateja na wasio wateja. Kuchukuliwa kwa huduma hiyo imekuwa ya kushangaza machoni mwa watumiaji tangu kuanzishwa mwezi uliopita." Tumekuwa tukipokea maombi kadhaa ya kuanzisha maduka ya Akiba Wakala kutoka maeneo tofauti nchini ambapo huduma hazijatolewa. Hii inaonyesha kuwa huduma imekuwa ya kuvutia kwa umma kwa ujumla," alisema Saria.

Katika kuongeza ufanisi wa benki hiyo, alisema ipo mbioni kufungua ukurasa mpya wa kibiashara kwa kujenga mfumo thabiti wa utoaji huduma kidijitali baada ya kupata mwekezaji wa kimkakati ambaye ni Benki ya Taifa ya Malawi (NBM).

# Waziri aielekeza Chemba kuandaa mpango kabambe

**Na Munir Shemweta,** CHEMBA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameitaka Halmashauri ya Wilaya ya Chemba mkoani Dodoma kuanza mikakati ya kuandaa mpango kabambe wa ardhi.

Mabula alisema hayo wakati wa ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi katika mkoa wa Dodoma.

Alisema wilaya za Chemba, Chamwino na Bahi ziko katika uso wa Jiji la Dodoma, hivyo ni lazima ziwe na mipango katika upangaji miji ili kuepuka ujenzi holela kushamiri.

"Bila kuwa na mpango kabambe huwezi kuwa salama, mko katika high way (barabara kuu) halafu mji umekaa tu bila kuwa na mpangilio na Chemba inaweza kunufaika na makao makuu," alisema Dk. Mabula.

Aliitaka Halmashauri ya Wilaya ya Chemba kuanza utaratibu wa kuandaa mpango huo kwa kuandika andiko la kuomba fedha wizarani ili kupanga, kupima na kumilikisha maeneo yake.

Aidha, aliitaka kuanza kuandaa pia maeneo kwa ajili ya uwekezaji kwa kuyapima ili wawekezaji watakapokuja wasipate tabu ya kupata maeneo.

Alisema, halmashauri hiyo ikiandaa maeneo ya uwekezaji mapema, itakuwa ni fursa kwa wawekezaji kutohangaika wakati watakapoenda kuwekeza wilayani humo.

Hata hivyo, alisikitishwa na Idara ya Ardhi katika halmashauri hiyo kuandaa hati chache katika kipindi cha mwaka mmoja ambapo halmashauri hiyo imeandaa jumla ya hati 120.

"Huwezi kuandaa hati 120 kwa mwaka mzima na hii haiwezekani na nataka kila mwezi mwandae hati zisizopungua mia moja na nakuagiza kamishna mwezi ujao nipate mwenendo wa hati katika halmashauri hii," alisema Dk. Mabula.

Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Dodoma, Thadei Kabonge, aliwataka watendaji wa sekta ya ardhi kujipanga na kuhakikisha wanafanya kazi kwa bidii kwa lengo la kumilikisha maeneo mengi ili kuiongezea serikali mapato kupitia kodi ya pango la ardhi.

# Uingereza kuisaidia Tanzania kukabiliana athari za tabianchi

Na Gwamaka Alipipi

BALOZI wa Uingereza nchini, David Concar, amesema Serikali ya Tanzania imepiga hatua katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, kwamba Uingereza itakuwa bega kwa bega katika kusaidia juhudi hizo.

Amesema Serikali ya Tanzania imechukua hatua nzuri katika mapambano ya uhifadhi wa mazingira, hivyo sekta binafsi nazo zinapaswa kuiunga mkono serikali katika kufanikisha dhamira iliyowekwa.

Aliyasema hayo jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano uliowakutanisha wafanyabiashara kutoka Jukwaa la Maofisa Watendaji Wakuu wa kampuni (Ceo roundtable), waliokuwa wakijadili mchango wa sekta binafsi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

"Nimesafiri maeneo mengi hapa Tanzania, mabadiliko ya tabia nchi bado ni tatizo japokuwa serikali imekuwa ikipambana kukabiliana nayo. Jambo hili tunahitaji kukabiliana nalo kwa pamoja, jamii, sekta binafsi kwa sababu hali ya uchafuzi wa mazingira na mabadiliko ya hali ya hewa duniani siyo nzuri," alisema Concar.

Alisema Uingereza inachukua hatua kubwa katika mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi, hivyo nchi zilizoendelea nazo zinapaswa kuchukua hatua ya kupunguza athari zitokanazo na hali hiyo.

Concar alisema: "Hatuwezi kufanya lolote pasipo ushirikiano, kila nchi inapaswa kushirikiana katika kupunguza athari hizo, hata jamii pamoja na sekta binafsi nazo zinapaswa kuingia katika mapambano haya."

Mwenyekiti wa Jukwaa la Ceo roundtable, Sanjay Rughani, alisema wafanyabiashara wanapaswa kufanya juhudi za kuhakikisha mabadiliko ya tabia nchi hayaleti athari kwa jamii.

"Tuwe mstari wa mbele katika mapambano ya kuhifadhi mazingira, tushirikiane na serikali pamoja na jamii, tunataka Tanzania iwe mstari wa mbele katika mapambano, sisi Ceo roundtable tumejitolea kuhakikisha ifikapo mwaka 2030 athari za mabadiliko ya tabia nchi iwe sifuri, pia tutahakikisha tunatoa elimu kwa jamii," alisema Rughani.

Alisema pamoja na kuongezeka kwa umuhimu wa ajenda ya mabadiliko ya tabianchi, Jukwaa la Ceo roundtable linatambua fursa kwa viongozi wa biashara kuwa mstari wa mbele kuwajibika kwenye masuala yanayoathiri mazingira na hali ya hewa.

Rughani alisema: "Jioni hii, Ceo roundtable imewakutanisha viongozi wa biashara na wadau wengine kujadili jukumu la sekta binafsi katika kuendesha agenda ya mabadiliko ya tabianchi kuelekea maendeleo endelevu. Kupitia nguzo yake ya biashara na uendelevu, Ceo roundtable inaunga mkono mipango inayolenga uendelevu wa mazingira."




Mwakilishi kutoka Huawei Tanzania, Yohana Mathias (kushoto), akimkabidhi cheti Catherine Teodor, mmoja wa washiriki mafunzo ya uchakataji wa data kubwa yaliyotolewa jijini Dar es Salaam na Huawei Tanzania kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya TEHAMA. Kulia ni msimamizi wa shughuli za uendeshaji wa TEHAMA wa tume hiyo, Mhandisi Jasson Ndanguzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kutokwa damu baada ya kujifungua kunavyochangia vifo vya wanawake

Na Christina Mwakangale

ASILIMIA 26.3 ya vifo vya kinamama nchini vinasababishwa na kutokwa damu nyingi mara baada ya kujifungua.

Takwimu za vifo vya uzazi za Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto zilizokusanywa kutoka Januari hadi Desemba mwaka jana, zinaonyesha asilimia 26.3 ya vifo vingi vilisababishwa na kutoka damu nyingi baada ya kujifungua.

Akizungumzia kampeni hiyo juzi Septemba 21, 2021, Mkuu wa Idara ya Ukusanyaji Damu katika Mpango wa Taifa wa Damu Salama, Dk. Avelina Mgasa, alisema kauli mbiu ya kampeni za mwaka huu ni 'Changia Damu Kuokoa Wanaoleta Uhai Duniani'.

Dk. Mgasa alisema imezinduliwa kampeni ya kitaifa ya kuihamasisha jamii kuchangia damu ili kuokoa vifo kwa wajawazito vinavyotokana na uzazi.

"Kampeni hii inalenga kuihamasisha jamii kujitolea kutoa damu kwa hiari ili kuokoa maisha ya kinamama wajawazito ambao wanatumika kama chombo cha kuleta uhai duniani," alisema Dk. Mgasa.

"Kaulimbiu inatupa hamasa na kuihamasisha jamii kujitolea kuchangia damu kwa hiari, ili kuongeza upatikanaji wa damu ya kutosha na salama ambayo itasaidia kuokoa maisha ya kinamama ambao hupoteza maisha kila siku kutokana na matatizo ya uzazi na wakati wa kujifungua."

Dk. Mgasa alisema kampeni hiyo iliyozinduliwa katika kanda zote saba za kukusanya damu nchini zilianza Jumatatu wiki hii, na imelenga kukusanya chupa za damu 19,514 kutoka kwenye timu 226 zilizopo nchi nzima ambazo ni asilimia tatu ya malengo yao ya damu kwa mwaka.

Aidha, Dk. Mgasa alisema kampeni ya mwaka huu inailenga jamii kuwa wachangiaji wa damu kwani asilimia 80 ya damu inayokusanywa nchini inakusanywa kutoka kwa wanafunzi na vijana wanapokuwa shule za sekondari na vyuoni.

## Tume TEHAMA, Huawei zawapa ujuzi wataalamu

Na Mwandishi Wetu

TUME ya TEHAMA kwa kushirikiana na Kampuni ya Huawei Tanzania zimetoa mafunzo kwa wataalamu 19 kutoka katika sekta ya umma na binafsi kwa lengo la kuwaongezea ujuzi wataalamu wazalendo.

Akifunga mafunzo hayo jijini Dar es Salaam jana, mwakilishi wa uongozi kutoka Kampuni ya Huawei Tanzania, Yohana Mathias, alisema mafunzo hayo ni chachu katika kuendelea kuibua ubunifu mpya kwenye sekta ya TEHAMA.

Alisema mafunzo hayo yaliyofanyika kwa siku saba ni kielelezo tosha namna Huawei inashirikiana na serikali katika kunoa Watanzania wengi kumudu kufanya kazi kubwa zinazohusu uchakataji wa data badala ya kwenda kuchukua wataalamu kutoka nje ya nchi.

"Huawei kila mara tumekuwa tukishirikiana na serikali kutoa mafunzo ya aina hii kwa sababu tunaamini TEHAMA ni sekta ambayo inakua kwa kasi, hivyo ni vema kuwaandaa Watanzania kuendana na mapinduzi ya nne ya viwanda duniani," amesema.

Msimamizi wa shughuli za uendeshaji wa TEHAMA kutoka Tume ya Taifa ya TEHAMA, Mhandisi Jasson Ndanguzi, pamoja na kuishukuru kampuni ya Huawei kwa jitihada hizo, alisema mafunzo hayo ni moja ya mikakati ya tume hiyo katika kutengeneza mpango wa Taifa wa miaka mitatu wa maendeleo.

Alisema mpango huo pia unalenga kuwasajili wataalamu wa TEHAMA, pamoja na kuwaendeleza kwa kuwajengea uwezo ili kuenenda na maendeleo ya TEHAMA duniani.


"Ndani ya mapinduzi ya nne ya viwanda kunatumika teknolojia ya hali ya juu ndio maana tume tumeona kuna haja ya kuwajengea uwezo mpya kwa sababu inawezekana teknolojia wanazotumia zinapitwa na wakati...na hii ndio sababu tunawashukuru sana wenzetu wa Huawei kwa jitihada zao katika kufanikisha mpango huu."

"Kwa hiyo mbali na mafunzo tunawasajili ili tuweze kujua tuna wataalamu wangapi kama nchi, na wataalamu hao kila mwaka na kila siku wanajiendeleza kivipi ili kama nchi tujue tuna ujuzi kiasi gani na tunaweza kunufaika vipi na fursa zilizopo kwenye TEHAMA," alisema.

Aliongeza kuwa serikali imekuwa ikiboresha miundombinu ya TEHAMA, lakini sasa inaanza kuweka mkazo kwenye uboreshaji wa rasilimali watu ili Tanzania iwe na watalaam wa kutosha. "Kwa hiyo mafunzo haya yanahusu big data analysis (uchakataji wa data kubwa) ambazo zinaweza kusaidia kutoa taarifa sahihi na kuwezesha kufanya maamuzi sahihi ya kiutawala na kimaendeleo," alisema.

Alisema tangu wazindua mpango wa mafunzo hayo Aprili mwaka huu, jumla ya washiriki 157 wamefaidika na kuongezewa ujuzi katika maeneo ya uchakataji wa data kubwa, usimamizi wa miradi ya TEHAMA, Cyber security na mafunzo mengine.

ama
ALHAMISI SEPTEMBA 23, 2021
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Simulizi ya mama anayetokwa damu muda wote na kuibuliwa tiba sahihi**



Ukurasa 13

Rais Samia aendeleza ya hali hewa aliyoanzisha Kikwete AU



Ukurasa 14

**Mtaalamu aainisha namna shida nguvu kiume zinavyoitesa jamii**

# Tanzania inao wagonjwa wenye maradhi kifua kikuu sugu 1600

**Na Yasmine Protace**




Kliniki zinazotembea, zilipozinduliwa mjini Dodoma, mwezi huu, moja ya hitaji lake kuu ni kutibu kifua kikuu. **PICHA: MTANDAO**

UGONJWA wa kifua kikuu ni hatari na imekuwa ikipoteza uhai watu wengi. Ni kawaida yake kuwa asili ya kukibilia mahali mapafu yaliko, lakini madhara yake hufika mbali zaidi, ikiathiri sehemu mbalimbali za mwili.

Maradhi kifua kikuu yanasambazwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine, kupitia hewa na hasa mgonjwa anapokohoa, kupiga chafya au mate yake yakiwa hewani. Haina tofauti sana na maradhi kama corona yanayotangazwa

Katika mustakabali wa kiafya kwa jumla, maambukizi mengi huwa hayana na madhara, baada ta tiba kuanza. Mara zote ni kawaida kifua kikuu kinacholeta madhara kwa mgonjwa ni pale anapokuwa na kikohozi sugu na baadhi kufikia hatua ya kukohoa damu, sambamba na kutopatwa na homa za usiku, huku kiafya anakonda zaidi.

Katika mikakati ya kupambana na maradhi hayo, serikali iliamua kujizatiti kwa kuwekeza kiasi cha fedha Sh. bilioni 97 kwa ajili ya kupambana na maradhi hayo, ikijumuisha mkakati ya kuimarisha huduma za afya vijijini na kupata takwimu sahihi.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk.Godwin Mollel, wakati wa uzinduzi wa Muungano wa Wadau wa Kupambana na Kifua Kikuu Tanzania, ulioshirikisha wabunge, viongozi wa dini taasisi na zingine, alisema serikali inatarajia kuwafikia wengi kwa kutumia magari ambayo ni vituo vya utabibu.

Kwa mujibu wa Dk. Mollel, ni namna inayoenda kumaliza shida ya ugonjwa huo na kutoa elimu ya moja kwa moja kwa jamii ya chini, mtazamo ukiwa ni kutokomeza matarajio hayo ifikapo mwaka 2030, wakiamini litafikiwa.

Kuhusu muswada wa Bima ya Afya kwa Wote, Naibu Waziri anasema kwa umeshaiva, kwani hadi tarehe za hivi karibuni ulishatoka mikononi mwa Kamati ya Makatibu Wakuu na sasa unapelekwa kwenye Baraza la Mawaziri, ili waupitie na kuuwasilisha bungeni Novemba, mwaka huu.

Dk. Saitole Laizer aliyemwakilisha Mganga Mkuu wa Serikali, anasema ni ugonjwa unaoendelea kuwa tishio nchini, ingawa bado kuna watu wengi wasiojua hatari yake katika kuua na inatakiwa juhudi za makusudi kuukabili kwa namna ya haraka.

"Vipimo vinaonyesha, kati ya watu 133,000 wanaofikiwa kwa ajili ya vipimo vya TB (kifiaa kikuu), 227 hukutwa na maambukizi ya ugonjwa huo ambao kwa sasa Tanzania ina jumla ya wagonjwa wenye TB sugu 1600 nchini kote, 400 waligundulika mwaka jana pekee," anasema Dk. Saitore

Hata hivyo anapataja pagumu pengine ni namna ya kuwafikia baadhi ya makundi yaliyo hatarini na ugonjwa huo, ikiwamo la watumiaji dawa za kulevya na wanaotafuta ulevi kwa namna ya kujidunga sindano, kwamba wanaingia nao hatarini.

"Serikali imetupatia fedha nyingi ambazo zimefanikisha kununua magari mapya matano yatakayofanya kazi hadi vijijini kwa ajili ya vipimo vya kwa watu wanaoshindwa kufika hospitalini, hivyo mapambano haya yanatakiwa kuwa endelevu kwa nguvu na kwa kila mmoja wetu," anasema.

Akizindua muungano huo, Spika wa Bunge, Job Ndugai, anasema kuwa TB ni miongoni mwa magonjwa yanayoua kwa wingi Tanzania na duniani ambayo hayatakiwi kufanyiwa mchezo katika mapambano yake.

Spika Ndugai, anawataka Watanzania kujihadharisha na hata kuchukua hatua wanapoona kuna za dalili za maradhi hayo, kwani ni ugonjwa unaoweza kumpata yeyote na wakati wowote, hivyo anaelekeza ombi lake ni taasisi za usimamizi kuwekeza fedha zao kwa vyombo vya habari, ili elimu ya ugonjwa huo ipelekwe hadi vijijini.

AFYA

MAGEUZI HOSPITALINI MUHIMBILI...

# Simulizi ya mama anayetokwa damu muda wote na kuibuliwa tiba sahihi

**Na Mary Geofrey**

• Mwezi analazwa mara 2 hadi 3 • Kila siku dawa za Sh. 130,000 • Mashine, vidonge maalum rasmi




Mwanahamisi Abdallah (katikati), alipozungumza na waandishi wa habari kuelezea afya yake. Kulia na kushoto kwake ni madakatari bingwa wa Hospitali ya Taifa Muhimbili waliomsindikiza.
**PICHA ZOTE: MARY GEOFREY**

MWANAHAMISI Abdallah (33), ni mama wa watoto watatu, anayesumbuliwa na shida kiafya. Anatatizwa na shida ya kuvuja damu katika maeneo mbalimbali mwilini, hivyo analazimika kuongezewa damu kila baada ya wiki mbili.

Ni hali inayomuingiza katika wakati mgumu analazimika kutumia tiba ya vidonge viwili kila siku, ambavyo vina gharama kubwa, kila kimoja kinauzwa Sh. 65,000 ikimuweka katika bajeti ya tiba Sh. 130,000 kila siku.

Ni ugonjwa uliopewa jina la uloto, unaotokana na utete ulioko ndani ya mifupa kushindwa kutengeneza chembe nyekundu za damu,

Mama huyo anaiambia Nipashe, kwamba akiwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) anakotibiwa katika Kitengo cha Magonjwa ya Damu, tatizo hilo lilipatikana mwaka jana, alipokuwa na ujauzito wa mtoto wake watatu.

"Nikiwa na mimba ya miezi tisa, ndipo nilianza kutokwa na damu puani na sehemu nyingine za mwili, nikaenda hospitali ndipo nikafanyiwa vipimo na kubainika nina tatizo la mwili wangu kushindwa kuzalisha chembe sahani," anaeleza.

Mama huyo mkazi wa mkoani Tanga, anasema awali alikuwa anaenda hospitali akiwa na anavuja damu, ndipo alibainika inapungua na mara, wakaanza kumuongezea kabla ya kumhamishia MNH.

Anasema tangu ameanza kuumwa mwaka jana, tayari ameshaongezewa chupa 50 za damu na chupa 90 za chembe sahani na kuna wakati alilazwa mwezi mmoja, akaongezewa damu na kutumia dawa za gharama kubwa, hali iliyofanya deni kufika Sh. milioni tano.

"Mkurugenzi wa MNH alinisamehe deni lile, alinisamehe yule baba wa watu kwa sababu sina shughuli ninayofanya ya kuniingizia kipato," anasema Mwanahamisi.

Anaiomba jamii iwachangie wagonjwa wa aina hiyo, kwa sababu gharama za matibabu makubwa.

**SHIDA ILIYOKO**

Mwanahamisi anasema, magumu aliyokutana nayo ni kukosa wachangiaji damu akiwa wodini hata kwa siku nne, akisubiri watu wa kujitolea damu, hali iliyomuumiza kisaikolojia.

Anasema huduma hiyo, Bima ya Afya haitumiki kwenye dawa anazotumia, hali inayomfanya kuangukia gharama kubwa kujitibu.

Mwanahamisi anataja kigumu kingine, ni kwamba amelazimika kuhama kutoka nyumbani kwake Tanga, kuja mkoani Dar es Salaam kupata matibabu, akiwa karibu na iliko Hospitali ya Taifa Muhimbili.

"Inabidi niishi kwa ndugu, wiki mbili nalazwa hospitali wiki moja narudi kuishi kwa ndugu na ndio yameshakuwa maisha yangu, hadi hapo nitakapopandikizwa uloto," anasema.

**DAKTARI BINGWA**

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Damu na Mkuu wa Kitengo cha Magonjwa ya Damu wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Stella Rwezaura, anasema mwili wa Mwanahamisi unashindwa kutengeneza chembe mbalimbali za damu.

Anataja sababu kadhaa za mgonjwa kufikiwa na mkasa huo, ikiwamo mabadiliko ya mwili kushindwa kutengeneza chembe sahani. Hata hivyo, kinachomsibu Mwanahamisi hakuna sababu maalum iliyokwishatambulika,

"Unaweza kuta umepata mafua tu, mwili unaanza kupambana kwa ajili ya vile virusi hadi wanaanza kushambulia chembe sahani na kushindwa kuendelea kuzalishwa, ndipo mtu anaweza kupata tatizo hili," anaeleza Dk. Stella.

Anataja aina za chembe za damu ambazo mwili wa Mwanahamisi unaoshindwa kutengeneza, ni nyekundu, nyeupe za chembe sahani.




Mashine mpya na ya kisasa iliyoletwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, kuleta mageuzi kwa wanaoelemewa na tatizo la upungufu wa damu.

Bingwa huyo wa tiba, anasema tatizo la mama huyo sasa linamsababisha alazwe kila mwezi mara mbili hadi mara tatu, hali inayomfanya aishi katikia mazingira ya kuongezewa damu, chembe sahani na kupatiwa huduma kwa ajili ya chembe nyeupe.

"Kwa sababu mwili wake hauwezi kutengeneza chembe nyeupe, anaishi kwa kutengenezewa za wengine na ndio maisha yake, hadi pale tutakapoanza kupandikiza Uloto," anasema Dk. Stella.

Anaeleza zaidi kuwa tiba ya ugonjwa huo ni kupandikizwa uloto, hivyo wakati wanasubiri kumpandikiza anahitaji kuendelea kuongezewa damu kila wiki, kupewa dawa na kuongezewa chembe sahani kila zinapoisha.

Anasema kila mgonjwa anaporuhusiwa na kurudi hospitalini, hupokewa akiwa na chembe sahani mbili na kwa kawaida zinazotakiwa kuwa 150 hadi 450.

Dk. Stella anasema mgonjwa wake huyo mara nyingine hufika hospitalini akiwa na kiwango cha damu kwenye mwili (haemoglobin) wastani wa mbili, tatu na isiyozidi sita, akiwa ametokwa damu sehemu mbalimbali za mwili wake.

Anasema ni mgonjwa anayekuwa na namna fulani ya kama damu inaganda kwenye ngozi huitwa 'kuvilia' na anahitajika wachangiaji wa damu kati ya 12 hadi 18, ili kumuwezesha kupata dozi moja ya chembe sahani, itakayomsaidia kuzipandisha aache kutokwa damu.

"Akija na chembe sahani moja au mbili anahitaji kuongezewa ile mifuko ya chembe sahani si chini ya 18 au 24 na ili kupata dozi moja, anatakiwa kuwa na wachangiaji si chini ya 30.

"Wanaomchangia wanapaswa kutorudia baada ya miezi mitatu hadi minne,"anasema bingwa huyo, ukiwa ni mkasa wa mgonjwa mmoja, ilhali wapo wengi kama huyo.

**UJIO WA MASHINE**

Daktari huyo anasema, mashine mpya zilizonunuliwa na MNH aina ya (Spectra Optia) za kutoa tiba ya magonjwa zaidi ya 10 ikiwamo UVIKO-19, upandikizaji uloto na kuchukua damu utasaidia kupunguza kundi kubwa la watoa damu.

Anasema mashine hizo zenye thamani ya Sh. milioni 245 zitasaidia kuvuna chembe mama za kuzalisha damu (hematopoietic stem cells), mazao ya damu ikiwamo chembe sahani (platelets), chembe nyeupe (granulocytes) na utegili (plasma).

> **"Inabidi niishi kwa ndugu, wiki mbili nalazwa hospitali wiki moja narudi kuishi kwa ndugu na ndio yameshakuwa maisha yangu, hadi hapo nitakapopandikizwa uloto.**

**INAENDELEA UK.13**

MAZINGIRA

# Rais Samia aendeleza ya hali hewa aliyoanzisha Kikwete AU

**Na Peter Orwa**

JUZI Rais Samia Suluhu Hassan alitua jijini New York Marekani na kuweka rekodi ya namna ambavyo Tanzania inang'ara na mkuu wake wa nchi mwanamama.

Samia ni miongoni mwa viongozi wachache wanaohudhuria mkutano wa 76 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa jijini New York, ambao kwa sehemu kubwa unafanyika kwa njia ya mtandao.

Karibu viongozi 100 watahudhuria mkutano huo kupitia mtandao, baada ya kushauriwa wasieende New York, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kimataifa kupambana na janga la COVID-19, ambalo sasa limwekuwa la dunia, wenyeji wa mkutano Marekani wakiwa sehemu ya waathirika wakubwa.

Akizungumza alipowasili New York Jumapili iliyopita, Rais Samia, alisema atahudhuria vikao mbalimbali, lakini mkazo wake unaingia zaidi katika suala la mabadiliko ya hali ya hewa na jinsi Tanzania inavyokabiliana na janga hilo.

Rais Samia, ambaye atakuwa katika kikao cha Mkutano wa Baraza Kuu leo, anasema mbali na kuhudhuria mazungumzo mbalimbali ya Umoja wa Mataifa, amefuatana na ujumbe muhimu wa wafanyabiashara kwa ajili ya kukutana na wenzao wafanyabiashara wa Marekani.

Ni aina ya hatua ambayo imekuwa ikichukua nafasi kimataifa kutoka nchi nyingi, ikiwamo China imekuwa ikitoa mfano mara nyingi nchini Tanzania, ambako katika ziara zake kisiasa, wakiwa wageni wa marafiki zao Chama Cha Mapinduzi (CCM)



Rais Samia Suluhu Hassan akishiriki mkutano mkutano wa 76 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa jijini New York, Marekani. **PICHA: MTANDAO**

Suala la msisitizo ambao leo hii Rais Samia Suluhu Hassan 'anashikiia bango' imekuwa na mzizi mrefu.

Mnamo Juni mwaka 2014, katika kikao cha Umoja wa Afrika (AU), jijijini Malabo, Guinea ya Ikweta, dhana hii iliibuliwa na Mtanzania.

Kikao hicho kilipata ugeni wa ghafla wa aliyekuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Ban Ki Moon, aliyeomba faragha na Kamati ya AU iliyohusiana na hali ya hewa iliyokuwa chini ya Rais Jakaya Kikwete.

Ni aina ya faragha ambayo Ban Ki Moon, alitumia nafasi hiyo kuzishawishi nchi za Kiafrika kukubaki kuafikiwa Mkataba wa Paris kuhusu hali ya hewa.

Katibu Mkuu wa UN alisisitiza namna ulivyo na manufaa kwa Waafrika, huku akiwapa mfano linganishi kwamba waharibifu wa hali ya hewa kwa asilimia zaidi ya 70 ni nchi zilizoendelea kutoka kwenye viwanda vyao, shughuli zinazowanufaisha kiuchumi.

Aliwaambia, ni wakati huohuo Afrika haishiriki sana kuchafua hali ya hewa, lakini ndiye mwathrika mkubwa, hivyo angewashangaa sana kama wangeshabikia mwenendo huo wa kukataa mkataba wa kulinda hali ya hewa, pasipo kujua uhalisi wa mambo.

Hapo ndipo Mwenyekiti wa Kamati ya hali ya Hewa AU, Rais Jakaya Kikwete nilimshuhudia ukali wake dhidi ya Waafrika wenzake kukiuka kanuni za hali ya hewa kwa manufaa yao.

Bila kupepesa macho, aliwatamkia kwamba yeye na wenzake wachache kama Waziri Mkuu wa Ethiopia, Meginstu Haile Mariam, ndio walionekana kuwa mstari wa mbele katika harakati za hali ya hewa AU na viongozi wengi wa kitaifa hawakulipa uzito suala hilo na waliwakilishwa na mawaziri, pindi aliitisha vikao vya kamati yake kujadili mustakabali huo.

Ni kweli hata ushuhuda wa kikao hicho cha AU jijini Malabo, kulikuwapo wakuu wa nchi wengi, lakini kikao mahsusi cha hali ya hewa, baadhi waliwakilishwa na mawaziri ambao Rais Kikwete aliwalalamikia kwamba hawakuwa na uamuzi kamili.

Ban Kin Moon huku akiwaita Waafrika 'ndugu zangu' aliwataka kuwa mstari wa mbele kuifanikisha mafanikio hayo ya Mkataba wa Paris, kwamba wao ndio waathirika wakuu, pia wanufaika wachache.

Aliwanong'oneza kuwa Rais wa Marekani, Barak Obama, walishateta na hakuwa na shida, ila akamuahidi ampe muda kuwaweka sawa wenye viwanda nchini mwake, kwani ni jumuiya yenye ushawishi katika siasa za nchi yake.

Baada ya hapo, aliacha faragha ya kikao kikiendelea chini ya Rais Kikwete na mwakilishi wake, mwenyewe akiahidi kuwahi Ulaya, ambako alidokeza hao ndio wana hulka ya 'ubishi' katika kufanikisha mpango wake huo.

Hiyo ilikuwa maandalizi ya kikao cha Washington miezi mitatu baadaye, yaani - Septemba, 2014, ambako ilifanyika kwa mafanikio makubwa, hata kikao cha Paris mwaka uliofuata jijini Paris ulifanikisha Mkataba wa Paris.

Kwa maana hiyo, anachokifanya sasa Rais Samia, inapaka rangi mzizi ulioanza kufanyiwa kazi na Rais Kikwete, chini ya kofia mbili, uenyekiti wa Kamati ya Hali ya Hewa AU na Rais wa Tanzania, ambayo imebeba ajenda ya hali ya hewa kwa uzito sahihi, ikiendeshwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, ambako Mama Samia ni mwenyeji sana.

# Simulizi ya mama anayetokwa damu muda wote

INATOKA UK.12

Anasema, kupitia mashine hiyo mchangiaji wa chembe sahani mmoja, anaweza kumchangia damu ya kutosha na kupandisha kiwango cha chembe sahani zake kutoka sita hadi 90.

Daktari Stella, anaeleza awali walihitaji ndugu wengi wanaojitolea damu kuhimili kiwango hicho cha chembe sahani na bado mgonjwa alitumia hadi mwezi mmoja kupandisha chembe sahani alizoongezewa.

Anasema, mifuko sita ya chembe sahani ina uwezo wa kuongeza kiwango cha chembe sahani kwenye mwili wake kutoka sita hadi 10.

"Anasubiri tena umuwekee, anakaa kidogo zinashuka tena hadi tano na hapo unasubiri tena wachangiaji wengine tena ili wamuongezee damu," anasema Dk. Stella.

**UPANDIKIZAJI ULOTO**

Dk. Stella anawataja wahitaji ni wenye saratani za damu, selimundu kali isiyokubali tiba ya kawaida, ambayo miili yao haitengenezi chembe za damu.

Anasema wanatakiwa kutibiwa kwa kupandikizwa chembe za kupandisha damu kutoka kwa wagonjwa wenyewe na wanaoweza kupandikizwa kutoka kwa ndugu wa karibu, ambao vinasaba vinashabihiana.

Mtaalamu huyo anasemaa, kwa mgonjwa anayeenda kutibiwa nje ya nchi gharama yake inafika kati ya Sh. milioni 200 hadi 250, lakini anapotibiwa nchini inaangukia wastani theluthi moja, kati ya Sh. milioni 70 hadi 80.

Dk. Stella anasema wagonjwa waliofuata huduma nje ya nchi, walitumia gharama kubwa kujikimu na usafiri, mzigo ambao serikali ilibeba.

**IDADI YA WAGONJWA**

Dk. Stella anasema uhitaji wa wagonjwa kupandikizwa uloto ni mkubwa na kwa mwaka ni wahitaji kati ya wagonjwa 100 na 150 na kabla ya kupandikizwa, huwa wanaongezewa damu, chembe sahani na chembe nyeupe kila baada ya wiki mbili.

Anafafanua uhitaji wa damu upo kwa sababu kinamama wanaojifungua nao ni wahitaji wa kuongezewa damu, sambamba na wenzao wa ajali na upasuaji.

"Linapokuja suala la mahitaji ya damu siyo tu wagonjwa wa kitengo cha damu bali tunazungumzia wagonjwa wa hospitali nzima na hospitali za jirani zinazowazunguka," anasema Dk. Stella.

Kwa mujibu wa Dk. Stella, wanahitaji 'Unit' 600,000 na kinachopatikana ni moja ya tatu ya mahitaji yote, lakini kuwapo mashine hizo kutasaidia kiwango cha damu zinazokusanywa kuongezeka.

Dk. Stella anaitetea mashine hiyo kuwa bora na ya kisasa na anasema kuna mafundi stahiki wa kuhudumia na kunapokuwa na uhitaji mkubwa, kuna wakala wanaowaleta mafundi wa kigeni.

AFYA

# Mtaalamu aainisha namna shida nguvu kiume zinavyoitesa jamii

- Kuna yanaowakuta wakisaka mbadala
- Ukiukwaji kanuni za mlo nayo janga

**Ally Mlanzi na Donald Lukele,**

TUDARCO

UKOSEFU wa nguvu za kiume ni njia panda inayowakabili watu wengi hususan vijana. Ni suala linalochangia migogoro mingi na hata kuvunjika ndoa, huku wengine wakijitoa uhai, wanapojihisi kuona hawana thamani ya kuishi kutokana na udhaifu huo

Omary (jina la pili tunalo) mwenye umri wa miaka 28, ni miongoni mwa vijana wenye magumu hayo, anayeiambia Nipashe kwamba anachokutana nacho sasa, ni ugumu wa ama kufaidi au kunufaika na tendo la ndoa anapokutana na mwenza wake.

“Kiukweli sijui kwani nikiona hali hii mpaka sasa, inanipa tabu hasa ninapokutana na mpenzi wangu katika tendo la ndoa... nimeanza kuwa na hofu hata ya kumpoteza mwenza niliye nae sasa,” anafafanua

Daktari Ramadhan Suleiman, ni mtaalamu kutoka Kituo cha Afya cha Madina Herbal Clinic, kilichopo Upanga Dar es Salaam, anayelifafanua hilo kwa kutaja sababu mojawapo ya kupungua nguvu za kiume, kuwa mfumo wa maisha wa mtu na vyakula vinavyotumiwa na wengi kwa sasa.

Anasema, kutokana na hali ya maisha ilivyo sasa, kuibuka mfumo wa kutozingatiwa milo ya inayopaswa, watu wengi wamekuwa wakila vyakula vyenye madhara kwenye miili yao.

Katika hilo, anataja athari katika utendaji kazi wa mwili, ikiwamo mzunguko wa damu na madhara mengineyo, ikiwamo upungufu wa nguvu za kiume.

“Vyakula kama nyama za makopo, kuku wa kisasa na mayai yake, vyakula vyenye mafuta mengi kama chipsi, sambusa, karimati, tambi na vinywaji vya viwandani vyenye sukari nyingi kama soda. Pia, bia huathiri sana mzunguko wa damu,” anasema.

Dk. Suleima anaendelea na somo lake: “Inasababisha mtu kutokuwa na uwezo wa kushiri kitendo la ndoa kwa muda mrefu kutokana na damu yake kutozunguka ipasavyo,”

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, magumu humkabili mtu kwa sababu nyingi za kimaumbile, zikiwamo za kukusudia, mwanamume anafanya tendo la ndoa pasipo mwenza.

Pia, anataja mtu anapopatwa na uvimbe katika mfumo wa uzazi, kuwa na ugojwa wa ngiri, matumizi makubwa ya dawa zenye kemikali ya kutibu magonjwa kama vile kansa, vidonda vya tumbo, kisukari na moyo.



Ndio sura halisi ya uhusiano, unaohusu dodoso za kimapenzi. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> **Vyakula kama nyama za makopo, kuku wa kisasa na mayai yake, vyakula vyenye mafuta mengi kama chipsi, sambusa, karimati, tambi na vinywaji vya viwandani vyenye sukari nyingi kama soda.**



Daktari huyo ana ushauri kwamba, bado mtu anaweza wanaweza kujiepusha kuingia katika magumu hayo kwa kuzingatia mfumo sahihi wa maisha, ikiwamo katika mlo na kufanya mazoezi sahihi na wakati stahiki.

Anasema, kwa sasa takwimu zinaonyesha kuwa watu wenye umri kuanzia miaka 20 hadi 40 ndiyo waathirika wakubwa wa shida hizo na wengine wanahisi kurogwa pasipo kufahamu mzizi wa maisha waliojiwekea na athari zilizoko.

“Leo hii watu wengi hula chipsi na soda takribani siku 14 katika mwezi. Hii ni hatari, kwani wanajaza mafuta na sukari mwilini, wanaleta madhara mengi ikiwamo kushindwa kuhimili tendo la ndoa na wengine hukosa kabisa hamu ya tendo la ndoa,” anasema Dk. Ramadhan.

Mtaalamu huyo anasema ishara zilizopo ni kama mtu anajihisi dalili za kushindwa kuhimili tendo la ndoa kuanzia muda dakika tano au anachoka sana baada ya tendo hilo.

Mengine anayoyataja yanajumuisha pale baada ya tendo ndoa mtu anakosa hamu ya kurudia tena; kukosa pumzi na uchangamfu wa mwili katika utendaji; nyenzo za kiume kukosa uimara au kushindwa kabisa, vyote vikiangukia kwamba uwezo wake wa afya ya uzazi za mtu upo matatani.

Ili mwanamume awe dhahiri katika kuhimili tendo la ndoa, eneo lake la faragha husika linapaswa kuwa imara na inavyostahili katika hali ya utayari na lazima apate mawasiliano ya kupokea damu inavyotakiwa.

Pia ni lazima mfumo wa misuli unapaswa kuwa vizuri kupokea damu, kwa maana damu iwe na uwezo wa kusafiri kwenye misuli ya mwili kutokana na vyakula watu wanavyokula.

Inaelezwa kinachotokea kiafya, mifumo ya damu inashindwa kufanya kazi ipasavyo na kufanya sehemu inayotumika kwa tendo la ndoa kubaki na ulegevu na hapo daktari anaseme, ndio panapoibua mada, watu wakilalamika wamelogwa.

### USHAURI WAKE

Dk.Ramadhani anasema, ili watu waepukane na hali hiyo ngumu na kurejea uimara wa asili, wanapaswa kula vyakula vya asili kama mboga za majani, matunda ili mwili upate virutubisho stahiki na wakati huohuo wanaepuke kula vyakula vyenye mafuta mengi na vinywaji vyenye sukari nyingi.

Pia, anasisitiza haja ya watu kufanya mazoezi ya kila mara wajiimarishe misuli yao na kuwawezesha kuwa na mzunguko mizuri ya damu mwilini, waepuke kushiriki tendo la ndoa kwa njia mbadala pasipo kuwa na mwenza.

Anataja lingine, ni pale mtu anajihisi hayupo sawasawa, aende mahara penye huduma za afya, akitaja mahsusi mfano wa anapoona upungufu katika mfumo wake wa uzazi, ili waibue chanzo cha tatizo na kumpata tiba fasaha, badala ya kuegemea njia zisizothibitishwa kitaalamu.



## Wawekezaji sasa wapewa ahadi mazingira mazuri

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amewahakikishia wawekezaji wanaowekeza mkoani humo kuwa serikali imeweka mazingira mazuri kwao, ili kuchangia kuinua uchumi wa eneo hilo.

Mtaka aliyasema hayo juzi kwenye ziara ya kukagua ujenzi wa kiwanda cha mbolea cha Inracom kinachojengwa na mwekezaji kutoka Burundi.

Mtaka alisema wataendelea kuhakikisha Dodoma unakuwa mkoa wa kwanza kwenye unafuu kiuwekezaji kutokana na serikali kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji.

"Watu kama wana fedha waje kuwekeza jijini Dodoma, ili mji wa Dodoma ushamiri na kukua, sisi kama serikali tutabeba dhamana ya kuwaondolea wawekezaji urasimu kwenye Ofisi za Serikali," alisema Mtaka.

Alibainisha kuwa kuna eneo la hekari 3,000 limetengwa kwa ajili ya uwekezaji katika eneo la viwanda mkoani humo.

Kuhusu ujenzi wa kiwanda hicho, alitaka kuwapo na uwiano kati ya raia wa kigenina wazawa kutokana na taarifa kuonyesha kuna wafanyakazi 500 huku raia wa Burundi ni 200.

"Suala hilo liangaliwe kwani sheria iko wazi, pia suala la vibarua kufukuzwa kiholela lifanyiwe kazi, Mkuu wa Wilaya alikuja hapa Ijumaana kuna taarifa vibarua 30 walifukuzwa ikiwamo wale waliouliza maswali jambo kama hili si jema," alisema Mtaka.

Kadhalika, aliagiza Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) kupanua barabara zote za eneo hilo kutokana na wenye kiwanda hicho hivi karibuni watahitaji kupitisha makontena 200 yenye mashine mbalimbali.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, aliwataka vibaruakufanya kazi kwa bidii.

Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe, aliwataka vibarua wanaofanya kazi za ujenzi kukiamini kiwanda, nauongozi wake ufikirie kuwapatia motisha ikiwamo vyeti na uwekwe utaratibu wa kuwa na msemaji.

Meneja wa mradi, Mhandisi Msafiri Dieudorine, alisema mradi huo ulianza Julai Mosi mwaka huu na wafanyakazi wote wana vibali vinavyotakiwa kwa mujibu wa sheria.

**Alibainisha kuwa kuna eneo la hekari 3,000 limetengwa kwa ajili ya uwekezaji katika eneo la viwanda mkoani humo.**

# Gwajima aagiza sensa ya magari programu za afya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, ameagiza kufanyika kwa sensa ya magari yanayotolewa kwa ajili ya programu za afya, baada ya kubainika hayafanyi kazi iliyokusudiwa.

Dk. Gwajima aliyasema hayo jana alipokuwa akikabidhi magari sita kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli za afya mazingira na usafi katika mikoa ya Kagera, Mara, Manyara, Tabora, Songwe na Mtwara

Alisema magari yanayotolewa kwa ajili ya programu hizo asilimia 75 yamekuwa yakitumika kwa kazi nyingine huku asilimia 25 tu ndio yanafanya kazi iliyokusudiwa.

"Kuna magari tunapeleka halmashauri yakafanye shughuli za afya unakuta asilimia 75 hayafanyi programu husika, asilimia 25 ndio kazi za afya na hapo unakuta gari katika kati ya asilimia 25, asilimia 10 lilikuwa gereji hapana, tunaanza sensa ya kwa kiwango gani magari yanayopelekwa kusimamia programu za afya yanatumikaje huko yanakokwenda."

"Hatusemi sekta ya afya isiwe na ushirikiano na sekta nyingine tunataka uwiano katika matumizi ya magari hayo na kazi gani linafanya kazi kusaidia sekta nyingine maana zote ni sekta za serikali," alisema.

Waziri huyo alisema suala hilo ni hoja ya ukaguzi kama magari yatafanya kazi asilimia 75 kwenye sekta nyingine huku afya likifanya kwa asilimia 15.

"Hali hii inakwamisha programu kutofikia malengo na serikali kujitetea matokeo gani imefanyika katika shughuli iliyokusudia," alisema.

Aliagiza kuwe na rekodi na kumbukumbu sahihi za matumizi ya magari kwa wakati wote.

"Nawakumbusha kufanya kazi kwa bidii ili programu hii ionyeshe matunda ya lipa kwa matokeo na tupate magari mengi zaidi," alisema.

Alifafanua kuwa wizara inatekeleza programu ya huduma endelevu za maji na usafi wa mazingira yenye lengo la kuboresha upatikanaji wa maji na huduma za usafi wa mazingira vijijini ambayo inatekelezwa mikoa 17 katika halmashauri 86 nchini.

Alibainisha sababu ya kuchagua mikoa hiyo kuipatia magari kuwa ni kwa kuzingatia vigezo vya hali duni ya upatikanaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira, kiwango cha umaskini na kiwango cha juu cha udumavu wa watoto.

"Kupitia programu hii mikoa na halmashauri zimeendelea kuboresha huduma za maji na usafi wa mazingira kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na jamii na kwa mwaka wa fedha 2020/21 halmashauri zimetekeleza katika vituo vya kutolea huduma za afya 873 nchini," alisema.

Aidha, Dk. Gwajima alisema serikali imenunua pikipiki 138 ambazo tayari zinatumiwa na maofisa afya ngazi ya kata kama sehemu na utatuzi wa tatizo la usafiri na yatanunuliwa magari mengine matano.

Awali, akizungumza kwa niaba ya kwa Mkurugenzi wa Kinga wa Wizara hiyo, Dk. Leonard Subi, Mratibu wa Kampeni ya Usafi wa Mazingira, Anyitike Mwakitalima, alisema magari hayo yamegharimu zaidi ya Sh. milioni 646.

Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichwale, alisema atahakikisha suala la sensa linafanyika ili kuhakikisha magari hayo yanatumika kwa lengo lililokusudiwa badala ya kazi nyingine.



Baadhi ya wafanyabiashara wadogo maarufu machinga, wakiendelea na shughuli zao huku wakiwa wamepanga bidhaa zao mbele ya maduka, kwenye eneo la barabara ya Oneway, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kanisa Anglikana kuadhimisha miaka 50

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika maadhimisho ya miaka 50, ya Kanisa la Anglikana Tanzania Septemba 27, mwaka huu, yatakayofanyika jijini Dodoma.

Maadhimisho hayo yatahudhuriwa na wachungaji zaidi ya 2,000.

Katibu Mkuu wa Kanisa hilo, Mchungaji Dk. Mecka Ogunde, alibainisha hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumzia na waandishi wa habari.

Dk. Ogunde alisema kanisa hilo mwaka huu linatimiza miaka 50 tangu kusajiliwa rasmi nchini kwa mujibu wa sheria.

"Tumepanga Jumapili ijayo ya Septemba 26, tutafanya ibada ya maadhimisho haya itakayoongozwa na Mkuu wa Kanisa hilo nchini, Maimbo Mndolwa," alisema.

Aidha, alisema Rais Samia atahutubia wachungaji zaidi ya 2,000 watakaoshiriki katika maadhimisho hayo ambapo pia kutakuwa na wawakilishi wa makundi mbalimbali.

"Wachungaji hawa zaidi ya 2,000 wataanza kuingia leo jijini hapa kwani kabla ya maadhimisho haya kutakuwapo na kongamano litakalo wajumuisha wachungaji wote wa Kanisa la Anglikana Tanzania," alisema Dk. Ogunde.

Akizungumzia kuhusu mafanikio ya kanisa hilo kwa miaka 50, alisema limekuwa na mchango mkuwa kwa taifa hasa katika masuala ya afya na elimu.

Alisema, kanisa hilo lilikuwa la kwanza kuanzisha kituo cha afya katika Wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma.

"Kama nilivyosema kanisa hili ndiyo lilikuwa la kwanza kuanzia huduma za matibabu, lakini tumekuwa tukitoa elimu kwa wananchi namna ya kujilinda na magonjwa mbalimbali ikiwamo UVIKO-19 ambapo tumetoa barakoa, vitakasa mikono na ndoo za kunawia mikono," alisema Dk. Ogunde.

Kadhalika, alisema katika sekta ya elimu kanisa hilo limekuwa mstari wa mbele kuanzisha shule kuanzia ngazi ya awali hadi vyuo vya kati na vyuo vikuu.

Vilevile, alisema kuwa kanisa hilo limekuwa mstari wa mbele kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia hasa ukeketaji kwa mabinti.

"Tumeanzisha vituo vya kuhifadhi watoto waliokimbia vitendo vya ukeketaji ambavyo vinawahifadhi kwa kuwapatia elimu pamoja na ulinzi katika mikoa ya Mara, Arusha, Manyara na Dodoma," alisisitiza.



# Wanaume watakiwa kupima maambukizi VVU

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANAUME wametakiwa kujitokeza kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kupima afya zao, ili kujua hali ya maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) badala ya kutegemea majibu ya wake zao.

Imeelezwa kwamba kutegemea majibu ya wake zao hakutoi takwimu sahihi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ukimwi, Kifua Kikuu, Dawa za Kulevya na magonjwa yasiyo ya kuambukiza, Fatma Hassan Tawfiq, aliyasema hayo juzi jijini Mbeya alipowaongoza wajumbe wa kamati hiyo kukagua afua mbalimbali za Ukimwi na dawa za kulevya.

Kamati hiyo ilifanya ziara ya kukagua afua hizo pamoja na kuangalia namna sahihi ya kukabiliana na maambukizi mapya ya VVU katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini pamoja na kutoa elimu ya kujikinga na VVU.

Tawfiq alisema baadhi ya wanaume wamekuwa wakikwepa kupima afya zao, kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kutojiamini kutokana na tabia zao na hivyo kusubiri wake zao wapime kwanza ili wayatumie majibu hayo kama ni sahihi kwa wote.

"Kama elimu ya upimaji itatolewa katika maeneo yote na watu wakajitokeza kupima hasa wanaume na wakawa waaminifu kwa wenza wao, kuna uwezekano hii vita tukaishinda na tukafanikiwa kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa maeneo yenye maambukizi kidogo ama kumaliza kabisa," alisema Tawfiq.

Alisema mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa mikoa ambayo inahitaji nguvu ya ziada kukabiliana na Maambukizi ya Ukimwi kutokana na takwimu kuonyesha kwamba bado kuna maambukizi makubwa.

Alisema kundi la watoto kwa sasa linaathirika zaidi na Ukimwi kutokana na kutokuwa na uwezo wa kujitetea wanapokutana na watu wazima ambao wanawabaka.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliiomba Kamati ya Bunge kufanya utafiti ili kujua sababu ya maambukizi kutoshuka katika baadhi ya mikoa ukiwamo Mkoa wa Mbeya ambao bado takwimu ziko juu.

Homera alisema mkoa huo bado takwimu zinaonyesha maambukizi yapo asilimia 9.3 na hivyo kuufanya bado kuwa wa tatu kitaifa ukitanguliwa na mikoa jirani ya Njombe na Iringa, na kwamba takwimu hizo ziko juu zaidi ya kile kiwango cha kitaifa.

Alisema tatizo la wanaume kutojitokeza kupima afya zao ni miongoni mwa vikwazo vinavyosababisha vita dhidi ya Ukimwi kutofanikiwa katika maeneo mengi.

"Tunawashukuru sana wadau wetu Walter Reed kupitia mradi wao wa Dreams, wanatusaidia kutoa elimu ya Ukimwi kwa makundi mbalimbali na kuviwezesha vikundi hivyo vya Dream kiuchumi ili kukabili maambukizi mapya," alisema Homera.

Aliwataka wanaume kujenga utamaduni wa kujiamini kupima afya zao ili wakibainika kuwa wana maambukizi waingizwe kwenye matumizi ya dawa za kufubaza virusi hivyo badala ya kuendelea kutumia majibu ya wake zao kama ndiyo majibu sahihi kwao.

Mbali na Mkoa wa Mbeya, pia kamati hiyo ilifanya ziara katika mikoa ya Songwe, Rukwa na Katavi.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (katikati), akizungumza na wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ukimwi, Kifua Kikuu, Dawa za Kulevya na magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza, Maofisa wa Walter Reed pamoja na baadhi ya watumishi wa Idara ya Afya ya mkoa huo, kamati hiyo ilipofanya ziara mkoani humo juzi, kufuatilia afua mbalimbali za Ukimwi na dawa za kulevya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Rungwe yaomba kujengewa barabara

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WAKAZI wa vijiji vya Kyobo Juu na Kyobo Chini vilivyoko Kata ya Ikuti wilayani Rungwe, wameiomba serikali kuwasaidia kujenga barabara yao waliyoitengeneza kwa mkono miaka mingi iliyopota ili magari yaweze kupita.

Wakizungumza kwenye mkutano wa hadhara ulioandaliwa na Mkuu wa Wilaya Rungwe, Dk. Vicent Anney, walisema kuwa barabara pekee inayoingia kwenye vijiji hivyo waliilima wenyewe kwa mikono miaka mingi iliyopita na haijawai kukwatuliwa na greda.

Deus Mwaijumba alisema kwa namna barabara hiyo ilivyolimwa na wazee wao miaka mingi iliyopita, magari hayawezi kupita na kuvifikia vijiji vyao, hivyo wanaomba msaada wa serikali iiboreshe ili iweze kupitika.

"Barabara hii ambayo ndiyo inaingia kwenye vijiji vyetu vya Kyobo Juu na Kyobo Juu haijawahi kutumiwa na magari tangu nchi ipate Uhuru, hii ni kwa sababu ililimwa kienyeji na wazee wetu kwa kutumia jembe la mkono miaka mingi iliyopita, tunaomba sasa Serikali itusaidie kuilima kwa greda ili magari yapite na kufika kwenye vijiji vyetu," alisema Mwaijumba.

Alisema katika vijiji hivyo wanazalisha mazao mengi ya biashara na chakula kama ndizi, Iliki, kahawa, magimbi na mihogo, lakini hawawezi kuyasafirisha kwa wingi kwenda kuyauza.

"Tunayo mazao yetu tunayolima kwa wingi, ingawa tunajua yana soko kubwa nje ya vijiji vyetu, lakini tunashindwa kuyasafirisha kwa wingi na hata wanunuzi wanashindwa kuja kuyanunua kwa sababu hakuna barabara.... baadhi yetu tunalazimika kuyabeba kichwani kwenda kuyauza ili tupate fedha za kujikimu, tunaomba tusaidiwe barabara kuondokana na kero hizi," alisema Mwaijumba.

Lucia James alisema ukosefu wa barabara pia unaathari kubwa kwa wanawake hasa wajawazito wanapohitaji kujifungua pale wanapotaka kwenda kwenye vituo vya afya.

Alisema usafiri pekee unaowasaidia wajawazito kwenda kujifungua kwenye vituo vya afya ni pikipiki, usafiri aliodai kuwa sio rafiki kwa baadhi ya wajawazito hasa ambao wanakuwa na matatizo ya uzazi.

"Baadhi ya wajawazito wanajifungulia njiani wakati wakienda kwenye kituo cha afya kutokana na kukosekana kwa usafiri wa gari, pikipiki ndio zinatusaidia, lakini kwa baadhi ya wanawake haziwafai na wengine wanajikuta wanapoteza watoto kwa kukosa huduma," alisema Lucia.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Mpokigwa Mwankuga, aliungana na wananchi hao kuomba msaada wa ujenzi wa barabara hiyo, akisema Serikali Kuu inapaswa kutenga bajeti ya kuwasaidia wananchi hao katika mwaka ujao wa fedha.

Mwakilishi wa Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) Wilaya ya Rungwe, Mhandisi Senyange Kayoka, alisema jukumu la wakala huo ni kufungua barabara kwenye maeneo yote ili wananchi wazitumie kwa shughuli za maendeleo.

Aliahidi kuwa katika mwaka ujao wa fedha barabara hiyo itakuwa ya kwanza kuingizwa kwenye bajeti ya TARURA, ili iweze kujengwa na kumaliza kero ya wananchi hao.

Akizungumza na wananchi hao, Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Anney, alisema atasimia kikamilifu kuhakikisha barabara hiyo inapitika kwa gari kwa manufaa na maendeleo ya wananchi wa vijiji hivyo.

Alisema barabara hiyo ikifunguka anaamini wananchi hao watapata maendeleo ya haraka kwa vile ni wazalishaji wazuri wa mazao ambayo yanapendwa na yenye soko la uhakika ndani nan je ya Wilaya ya Rungwe.

# Jiji latenga mil. 200/- ujenzi kituo cha afya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya, imetenga Sh. milioni 200 kutoka kwenye mapato ya ndani kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kata ya Ilemi, ambayo ni miongoni mwa kata ambazo hazina vituo.

Meya wa Jiji la Mbeya, Door Issa Mohamed, aliyasema hayo juzi wakati alipoongoza viongozi wa Jiji hilo kutembelea eneo kitakapojengwa kituo hicho na kisha kuzungumza na wananchi wa kata hiyo.

Mohamed alisema kituo hicho kinatarajiwa kujengwa kwa gharama ya Sh. milioni 524.6 kwa awamu ya kwanza, na kwamba fedha zitaendelea kutolewa kadri zitakavyokuwa zinapatikana kutoka kwenye vyanzo mbalimbali.

"Tutakijenga kituo hiki kwa kutumia utaratibu wa Force Account, hivyo nawaomba wananchi mjitokeze kujitolea kufanya kazi hapa maana utaratibu huu unataka sana ushiriki wa wananchi kwenye utekelezaji," alisema Mohamed.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Jiji hilo, Amede Ng'wanidako, aliwataka wananchi kuendelea kulipa kodi na tozo mbalimbali zinazotozwa na serikali ili fedha za kutekeleza mradi huo pamoja na miradi mingine zipatikane.

Alisema ili kufanikisha miradi, kila Mtanzania anatakiwa kuchangia kwa kulipa ushuru na kodi ili kuepuka kutegemea misaada kutoka nje ambayo kwa kiwango kikubwa huwa na masharti magumu.





# Vijiji 60 vyawasilisha ombi kupata umeme

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ZAIDI ya vijiji 60 vimewasilisha maombi ya kuunganishiwa huduma ya umeme ikiwa ni sehemu kufanikisha upatikanaji wa huduma hiyo kwa wananchi.

Waziri wa Maji na Nishati, Suleiman Masoud Makame, aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akitoa ufafanuzi wa mikakati ya serikali ya kuwapatia umeme wananchi kwa kuwaungia majumbani.

Waziri Makame alisema lengo la serikali ni kuona wananchi wananufaika na nishati ya umeme kwa ajili ya kuleta mabadiliko makubwa ya maendeleo ya kiuchumi na uzalishaji wa mazao mbalimbali.

Alisema juhudi zilizochukuliwa ni pamoja na kushusha bei ya viwango vya kuunganisha umeme majumbani kutoka Sh. 400,000 hadi kufikia Sh. 200,000.

Kiongozi huyo alisema viwango hivyo vinatarajiwa kushuka zaidi kutoka Sh. 50,000 hadi kufikia Sh. 30,000 hatua ambayo itawawezesha wananchi wengi kuunganisha umeme majumbani na kufaidi nishati hiyo kikamilifu.

Alisema kufuatia uamuzi wa shirika la umeme kushusha viwango vya kuunganisha umeme majumbani, tayari maombi mengi yamepokewa ya kuunganisha umeme kwa wananchi katika shehia mbalimbali Unguja na Pemba.

"Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) limeshusha kiwango cha kuunganisha umeme majumbani kutoka Sh. 400,000 hadi kufikiya Sh. 200,000 ambapo matarajio yetu makubwa viwango hivyo vitashuka zaidi hadi kufikiya Sh. 50,000 hatua ambayo itawawezesha wananchi wengi kupata huduma hiyo kwa maendeleo ya kiuchumi," alisema.

Aliongeza kuwa kwa sasa kazi kubwa inayofanywa na shirika la umeme (ZECO) kwa kushirikiana na viongozi wa shehia kukusanya maombi mbalimbali ya wananchi wanaohitaji huduma za kuunganishiwa umeme majumbani.

**Waziri Makame alisema lengo la serikali ni kuona wananchi wananufaika na nishati ya umeme kwa ajili ya kuleta mabadiliko makubwa ya maendeleo ya kiuchumi na uzalishaji wa mazao mbalimbali.**

# Waziri aona shida ushiriki wanawake katika uongozi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadid Rashid, amesema bado uwelewa ni mdogo kwa jamii kuhusu ushiriki wa wanawake katika uongozi.

Hayo yamo katika hotuba yake iliyosomwa jana kwa niaba yake na Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Kusini Unguja, Khamis Rubea Buheti, wakati wa mkutano wa uhamasishaji wa ushiriki wa wanawake katika uongozi uliofanyika katika viwanja vya Bungi mkoani humo.

Mkutano huo uliandaliwa na Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA) na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar kupitia mradi wa kuwajengea uwezo wanawake katika masuala ya uongozi.Rashid alisema mfumo dume uliotawala unamzuia mwanamke kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika kisiasa na kijamii.

"Tumekutana katika kipindi hiki tukiwa bado tunauhitaji mkubwa wakubadilishana mawazo kwa ajili ya kuijenga Zanzibar mpya itakayokuwa na ustawi na neema," alisema.

Mkuu wa Mkoa alisema wanahitaji kuwa na Zanzibar iliyoungana na tofauti za kijinsia zisiwe sababu ya kuyaacha makundi mengine nyuma katika nafasi za uongozi.

Mkurugenzi wa ZAFELA, Jamila Mahmoud, alisema wameanza kuzipitia sheria ambazo zinambana mwanamke kushiriki katika nafasi za uongozi.

Alisema lengo ni kumwezesha mwanamke kugombea nafasi za uongozi na kutoa elimu kwa jamii kuhusu ushiriki wa mwanamke katika harakati za kupata nafasi na kuchagua viongozi watakaoleta maendeleo.

"Matarajio yetu ni kuwafikia wanawake 6,000 kuwapa uelewa katika masuala ya uongozi, ukimwelimisha mwananmke umeielimisha jamii kwa sababu wanawake wana nafasi kubwa katika familia," alisema.

Mbunge wa Viti Maalum katika Mkoa wa Kusini Unguja, Mwatum Dau Haji, aliwataka wanawake kutokatishana tamaa kwa sababu wana uwezo wa kuwa viongozi huku akimtolea mfano Rais Samia Suluhu Hassan namna anavyochapa kazi.

Mwatum aliwataka wanawake wa mkoa huo kujitokeza kwa wingi wakati utakapofika wa kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kuanzia ngazi za chini hadi taifa.



Wakazi wa eneo la Kitope Maili 13, Mkoa wa Kaskazini Unguja, wakishuhudia ajali ya barabarani iliyoyahusisha magari mawili na pikipiki moja jana, ambapo watu watatu wamejeruhiwa. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Mwinyi asifu ushirikiano wa Zanzibar na China

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema tangu mwaka 1964, China imeendelea kuisaidia Zanzibar katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii, ikiwamo Sekta za Afya.

Aliyasema hayo juzi Ikulu Zanzibar alipozungumza na timu ya madaktari kutoka China waliomaliza muda wao baada ya kuwapo visiwani humo kwa muda wa mwaka mmoja wakifanya kazi katika hospitali mbalimbali.

Alisema nchi hiyo imeisaidia Sekta ya Afya kwa kuimarisha miundombinu, upatikanaji wa vifaa, dawa pamoja na kuwajengea uwezo watendaji wake.

Rais Mwinyi alisema katika kukabiliana na corona, nchi hiyo imesaidia utoaji wa mafunzo kwa wafanyakazi wa sekta za afya na utalii.

Kiongozi huyo aliishukuru na kuipongeza timu hiyo ya madaktari kwa kuunga mkono juhudi za serikali kwa kufanya kazi usiku na mchana ya kuwapatia huduma bora za afya wananchi visiwani humo.

Katika hafla hiyo, Rais Mwinyi alikabidhi zawadi kwa Balozi Mdogo wa China aliopo Zanzibar, Zhnag Zhisheng, pamoja na kuwavisha nishani madaktari hao.

Waziri wa Afya, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmeid Mazrui, alisema jamii haiwezi kuzungumzia historia ya Zanzibar bila kuzingatia mchango mkubwa wa China walioutoa sekta za kilimo, viwanda, miundombinu na afya.

Alisema timu hiyo iliomaliza muda wake katika Hospitali ya Rufani Mnazi Mmoja pamoja na Abdalla Mzee kisiwani Pemba imefanya kazi kwa ufanisi mkubwa kwa kuwapatia wananchi huduma bora na kuwajengea uwezo wa kiutendaji madaktari wazawa.

Alisema timu mpya inatarajia kuwasili visiwani humo hivi karibuni na itaendeleza kazi ya utoaji wa huduma bora za afya ikiwa ni hatua ya kuendeleza ushirikiano uliopo kati ya nchi hizo ambapo kila mwaka wamekuwa wakija.

Balozi Mdogo wa China, Zhisheng, alisema timu hiyo inafanya kazi chini ya miongozo ya serikali ya nchi hiyo na mbali ya kuhudumia hospitali Mnazi Mmoja, Abdalla Mzee, Kivunge na Chakechake ilikwenda vijijini kuwasaidia wananchi maskini walioshindwa kusafiri kufuata huduma za afya mijini.

"Katika kipindi hiki dunia ikikabiliana na ugonjwa wa corona, China imesimama pamoja na wananchi wa Zanzibar katika kukabiliana na ugonjwa huu ili kuleta ustawi wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii," alisema. Akitoa taarifa fupi ya kazi, Kiongozi Mkuu wa timu hiyo, Dk. Wang Yiming, alisema katika kipindi chote walichofanya kazi pamoja na madaktari wazawa wamefanikiwa kukabiliana na matatizo mbalimbali.

Alisema katika kipindi hicho walishughulikia kesi kadhaa za upasuaji pamoja na kutembelea maeneo mbalimbali ya Zanzibar kwa ajili ya huduma, dawa pamoja na kuwaongezea uwezo wa kiutendaji madaktari wazawa.

Kiongozi huyo alishukuru Wizara ya Afya na wananchi kwa utii na kuiunga mkono timu hiyo, akibainisha matumaini makubwa ya timu ijayo kufanyakazi vyema kwa ajili ya Wazanzibar.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Fatma Mrisho, alisema timu hiyo ni ya 30 ambapo miongoni mwao walikuwapo madaktari wa upasuaji, X-Ray, mionzi, huduma za watoto, magonjwa ya moyo, meno, tumbo, kuchoma sindano za kupunguza hisia pamoja na wakalimani.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA ENTEPRISES FINANCE LIMITED (EFL). KWA MAWASILIANO ZAIDI **TUPIGIE:0677 111 333 AU 0758 112 332**

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

KIWANJA KINAUZWA
KIWANJA KIPO KISUKURU JKT UKUBWA SQM 2252 KINA HATI, BEI MILIONI 60.
**MAWASILIANO 0786 857523 Au 0655 857523.**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

## KUPOTEA KWA VYETI



**MICHAEL DUMA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne Chenye index namba **S2476/0399/2012** Kilichotolewa na baraza la Mitihani la Taifa kupitia Mbagala Sekondari mwaka 2012. Taarifa ya Polisi **IRI/IRI/RB/458793/2021.** Cheti cha kidato cha sita Chenye index namba **SO.160/0738/2015** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Umbwe High School mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa Polisi. **Taarifa ya Polisi IRI/IRI/RB/458780/2021**

116471902

## KUPOTELEWA NA CHETI



Ndugu **RAMADHANI HAMISI** anatangaza kupotelewa na cheti chake cha kuhitimu BSC AGR ENGINEERING chenye **No. AGE/D/11/T/0012** kilichotolewa na SOKOINE UNIVERSITY OF AGRICULTURE (SUA) mwaka 2015. Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/KYA/RB/442124/2021.** Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye au apige simu namba **0682-655582**

116472102

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 121 OF 2021**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE PETER RAPHAEL MWARIA OF NZUGUNI WITHIN DODOMA CITY**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATIONFOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MONICA PAUL SHIRIMA**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn.369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Admirations made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 13th Day of October, 2021.
Dated at Dodoma this 21st day of September 2021

……………………………………
**RESIDENT MAGISTRATE**

116473202

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATED**
**OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**NO. 12 OF 2021**
**In the matter of Estate of the late HILDA HEMILIAN MALIPU**
**By ANTONY SHOMAR NGATIMWA**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above - named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.
Objection to the grant should be field on or before the **05 day of October .. 2021**
**Dated MOROGORO D/C this 20 day of 09 .. 2021**

**RESIDENT MAGISTRATE**

116473502

**IN THE COURT OF DISTRICT**
**DELEGET OF HAI**
**AT HAI**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 02 OF 2021**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE TUMSIFU THOMAS SWAI**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION OF THE ESTATE OF THE LATE TUMSIFU THOMAS SWAI**
**BY GLORIUS TUMSIFU SWAI**

**NOTICE OF MENTIONOF PETITION**
**Made under rule 68 (4)**

**TO: WHOM IT MAY CONCERN**
**TAKE NOTICE** that the above petition has been set for mention on 6th October before 2021 before Hon.T.G.Kombe - SRM.
**Dated at HAI this 9TH day of September, 2021**

……………………………………
**DISTRICT DELEGETE HAI**

116473902

**MAS & ASSOCIATES COMPANY LIMITED & COURT BROKER**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

KWA IDHINI NILIYOPEWA NA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MFAWIDHI MKOA WA KINONDONI-KIVUKONI NA MAHAKAMA YA MWANZO YA KINONDONI NITAKUWA NA ZOEZI LA KUFANYA MNADA WA HADHARA WA KUUZA NYUMBA NA KIWANJA .MNADA UTAFANYIKA KWA WAKATI KAMA RATIBA INAVYO ONYESHA

| NA | JINA | MALI INAYOUZWA | MAHALI | TAREHE | MUDA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | MADAI TALAKA NO 188/2018 JAZILA HASSAN DHIDI YA JALIA SELEMANI | NYUMBA | KIBAMBA MTAA WA MLOGAZILA | 7/10/2021 | KUANZIA SAA NNE KAMILI ASUBUHI (4:00) |
| 2. | MADAI NO 224/2019 VENGRISTA V. MHAGAMA DHIDI YA ASHA AMRI MWALIMU | NYUMBA | ENEO LA JITEGMEE KATA YA MABIBO | 8/10/2021 | KUANZIA SAA NNE KAMILI ASUBUHI (4:00) |

**MASHARTI YA MNADA:**
- UKAGUZI UNAANZA MARA BAADA YA TANGAZO HILI, MASHARTI YA MNADA:
- MNUNUZI ANATAKIWA KULIPIA ASILIMIA 25% SIKU YA MNADA NA ASILIMIA 75% SIKU KUMI NA NNE (14) TOKA SIKU YA MNADA NA HUKIKOSA KULIPA MNADA UTARUDIWA NA FEDHA ULIZOLIPA HAZITARUDISHWA.
- GHARAMA ZA KUBADILISHA JINA ZA MALI NI ZA MNUNUZI MWENYEWE
- MTEJA ATATAKIWA KULIPA FEDHA TASLIM SIO HUNDI.

**KWA MAWASILIANO**
**MAS & ASSOCIATES COMPANY LIMITED & COURT BROKER**
**SIMU: 0712 667989**
**WOTE/ MNAKARIBISWA**

116473302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Njombe**
**Kituo cha Njombe Mjini**
**Mkoa wa Njombe**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 82/2021**
**Katika Shauri la Mirathi ya IGINAS DICKSON PELLA……………MAREHEMU**

**Katika shauri la maombi ya kumteua msimamizi yaliyotolewa na VESTINA JOSEPH MLELWA…………….MWOMBAJI**

**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/ maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 11 mwezi wa 10 Mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa kabla au mpaka tarehe tajwa hapo juu.
**Zingatia:** Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 17 Mwezi wa 09 Mwaka 2021.

116472002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya Mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi NO.297/2021**

**Ombi la RAMADHANI IDDI KINANGU kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu SAIDI IDDI MBAWALA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 04/10/2021 kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 21/09/2021

116473002

**TEGEMEZA FINANCE AND COURT BROKER LTD**
**MBEZI BEACH P.O. Box 77593; SIMU: 0719 187677.**

## TANGAZO LA MNADA NA NOTISI

**Shauri la Madai No. 614/2020**
**Mdai – ZUHURA IDRISS**
**Dhidi ya**
**Mdaiwa – AZURE ONEH LIMITED**

116473402

Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na Mahakama Kuu kitengo cha kazi Dar es salaam tutakuwa na mnada wa hadhara tarehe 21/10/2021 kuanzia saa nne asubuhi.

| No. | Mali itakayouzwa | Mahali – | Muda – |
|---|---|---|---|
| | Gari aina ya IST – T 568 DLV | Mbezi Beach Bondeni | saa nne asubuhi |

**Masharti ya Mnada**
1. Mteja atalipa 25% itakayofikia bei ya mnada baada ya siku 14 atapaswa kumalizia kama atashindwa kumaliza atakuwa amepoteza haki zake.
2. Gharama zote zitakazojitokeza baada ya kununua mali kwenye mnada zitakuwa juu ya mnunuzi.

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com

116460202

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Vifo vyaongezeka ajali iliyoua ndugu watano

**Na Mwandishi Wetu**

IDADI ya vifo vya wanafamilia waliofariki dunia juzi kutokana na ajali ya gari iliyotokea Itewe, Inyala mkoani Mbeya, vimeongezeka na kufikia sita baada ya mtoto aliyejeruhiwa, Erick Mboya (13) kufariki dunia wakati akipatiwa matibabu kwenye Hospitali ya Kanda ya Rufani Mbeya (MZRH).

Juzi, watu watano wa familia ya Mboya walipoteza maisha kwenye ajali iliyohusisha magari matatu, huku ndugu watatu wakifariki dunia papo hapo na majeruhi wengine walifariki dunia wakati wakipatiwa matibabu MZRH.

Kwa mujibu wa msemaji wa familia hiyo, Simon Mboya, mazishi ya wanafamilia sita akiwamo mtoto huyo, yanatarajiwa kufanyika leo.

Alisema kati yao, wanne watazikwa eneo la Vwawa kwenye makaburi ya Makusu wilayani Mbozi, huku wawili wakitarajiwa kuzikwa Kata ya Igamba mkoani Mbeya.

Mboya aliwataja wanafamilia hao watakaozikwa leo kuwa ni Isabella Mboya (50), Severina Mgala (50), Joyce Mboya (48), Thomas Mboya (46), Magreti Mwasaka (23) na Erick Mboya (13).

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, katika taarifa yake juzi kwa vyombo vya habari, alisema ajali hiyo ilitokea juzi majira ya saa 11 alfajiri katika Kijiji cha Imezu, Inyala Mbeya Vijijini katika barabara kuu ya Mbeya-Dar es Salaam.

Kamanda Matei alisema ajali ilihusisha gari lenye namba za usajili T 616 DXE aina ya Scania, lililokuwa likiendeshwa na Blust Sevetu, likitokea Dar es Salaam, lililigonga kwa nyuma gari namba T 654 CRR na T 769 BZG lililokuwa limepata hitilafu na kupaki barabarani na kisha kugonga gari lingine namba T 544 BKW aina ya Raum lililobeba wanafamilia hao.

Alisema watu watatu walifariki dunia papo hapo na majeruhi wawili walifariki wakati wakipewa matibabu MZRH.

Alisema ndugu hao wa familia moja waliokuwa wakitokea msibani mkoani Mbeya, chanzo cha ajali kimebainika kuwa ni uzembe wa dereva wa gari namba T 616 DXE Scania, kutokana na kutokuchukua tahadhari wakati analipita lori lililokuwa limepata hitilafu barabarani na kwamba dereva aliyesababisha ajali alikimbia baada ya tukio.

Kamanda Matei alitoa wito kwa madereva kuwa waangalifu kwa kuzingatia sheria za usalama barabarani, udereva wa kujihami na kuacha mwendo kasi.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Simon Marwa Maigwa (katikati), akiwaonyesha waandishi wa habari jana, dawa za kulevya aina ya mirungi zilizokamatwa katika operesheni maalumu ya kupambana na usafirishaji, usambazaji na matumizi ya dawa hizo ikiwamo mihadarati, bangi, Cocaine na Heroin. **PICHA: JAMES LANKA**

## Benki Stanbic yaipa shule madawati 100

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BENKI ya Stanbic Tanzania imetoa madawati 100 yenye thamani ya Sh. milioni 12 kwa Shule ya Sekondari Mbabala mjini Dodoma.

Makabidhiano yalihudhuriwa na Mkuu wa Wilaya wa Dodoma, Jabiri Shekimweri. Msaada huo ni sehemu ya kampeni ya kitaifa inayoendelea ya 'STANBIC MADAWATI INITIATIVE' ambayo inakusudia kuchangia madawati 1000 katika shule tofauti nchini Tanzania na kutuoa mti mmoja kwa kila dawati ili kulinda ekolojia.

Shekimweri alisema madawati hayo yataboresha sana hali ya kujifunza kwa wanafunzi wa Mbabala na kutoa wito kwa watu wengine wenye nia njema kujitokeza na kujiunga na juhudi za kukabiliana na upungufu wa madawati uliobaki katika mkoa huo na nchi nzima.

"Kama tunavyojua sote, elimu ni chombo muhimu cha maendeleo. Tunaishukuru kwa dhati Benki ya Stanbic kwa kuunga mkono juhudi zetu za kuboresha upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia shuleni hapa. Tunaamini madawati haya 100 yatasaidia sana kuwezesha mamia ya watoto kuwa na mazingira mazuri yanayohitajika kwa kujifunzia, " alisema Shekimweri.

"Leo hii tumetoa madawati 100, lakini yataenda sambamba na miche 100 ya miti ya matunda ili kuhakisha tunalinda ikolojia na wanafunzi hawa wanafaidika na mazao yatakayotokana na miti hii," alisema Mkuu wa kitengo cha wateja binafsi wa benki hiyo, Omari Mtiga.

Mtiga aliongeza kuwa msaada huo unaendana na mpango wa benki hiyo uliozinduliwa hivi karibuni wa Stanbic Madawati ambao unakusudia kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa wanafunzi kote Tanzania na kuchangia kukuza maendeleo ya Watanzania kupitia elimu shirikishi na bora.

# Muhimbili yatumia bil. 60/- kwa misamaha matibabu

**Na Mary Geofrey**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH), imetumia zaidi ya Sh. bilioni 60 katika kipindi cha miaka 10, kama msamaha wa matibabu kwa wagonjwa wasiyo na uwezo.

Kati ya gharama hizo pia zinahusisha miili ya watu waliofariki dunia lakini ndugu zao hawana uwezo wa kulipia gharama za matibabu.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa MNH, Aminieli Aligaesha, alisema jana kuwa hospitali hiyo ambayo hutoa matibabu kwa wagonjwa takribani 4,000 katika mwaka 2020/21 walitumia Sh. bilioni 16 kwa ajili ya msamaha wa matibabu.

Alieleza mwaka wa fedha wa 2019/20 walitumia Sh. bilioni 14.1, mwaka 2018/19 walitumia Sh. bilioni nane, mwaka 2017/18 walitumia Sh. bilioni tano na mwaka 2016/17 walitumia Sh. bilioni sita.

Alifafanua zaidi kuwa, mwaka 2015/16 walitumia Sh. bilioni nane, mwaka 2014/15 walitumia Sh. bilioni nane, mwaka 2014/15 walitumia Sh. bilioni saba, mwaka 2013/14 walitumia Sh. bilioni tano, mwaka 2012/13 walitumia Sh. bilioni tatu na mwaka 2011/12 walitumia Sh. bilioni nne.

Alifafanua kuwa katika kusimamia utekelezaji wa msahama kwa wagonjwa wanatumia Maofisa Ustawi wa Jamii waliopo katika majengo yote ya kulaza wagonjwa katika hospitali hiyo ya taifa.

Aligaesha alisema wagonjwa wanaofika hospitalini hapo wakakosa fedha za matibabu, huelekezwa kwa maofisa ustawi wa jamii ili kujadili kwa pamoja namna ya kulipa au kusamehewa deni hilo.

"Wananchi ambao hawana bima za afya, suala la kuchangia huduma za matibabu ni muhimu sana kwa sababu zinachangia katika maendeleo ya hospitali katika kutoa huduma," alisema Aligaesha.

# SABABU SIMBA, YANGA KUBAKI DAR YAJULIKANA

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa zamani wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Madaraka Selemani amesema zamani watani wa jadi nchini walikuwa na tabia ya kuweka kambi Visiwani Zanzibar, Bagamoyo au Morogoro kwa ajili ya kujiandaa na mechi za 'dabi' ili kukwepa usumbufu kutokana na wachezaji wao wengi kuwa ni Watanzania.

**Simba na Yanga zinatarajia kukutana katika mechi ya kuwania Ngao ya Jamii itakayochezwa keshokutwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.**

Mkongwe huyo aliyezichezea pia timu za CDA ya Dodoma na Majimaji ya Songea, akipachikwa jina la 'Mzee wa Kiminyio', alisema kwa miaka ya karibuni, klabu hizo zimekuwa zikiweka kambi hapa hapa jijini kutokana na wachezaji wao wengi ni wageni, na hivyo kutokuwa na usumbufu wowote.

Madaraka alisema wachezaji wazawa hutembelewa na ndugu au marafiki mbalimbali na hivyo kuondoka umakini kuelekea mchezo huo muhimu ulioko mbele yao.

"Watu wanajiuliza ni kwa nini siku hizi Simba na Yanga zinaweka kambi hapa hapa Dar, wakati sisi enzi zetu wakati wa maandalizi wa mechi hizi ni lazima tutoke nje ya jiji, tuliondolewa Dar kwa sababu mkiwa kambini, wanakuja ndugu, jamaa, marafiki, kukutembelea na shida zilikuwa nyingi, hivyo wachezaji walilazimika wakati mwingine kuondoka kambini," Madaraka alisema.

Aliongeza uamuzi wa kuondoka jijini ulilenga utulivu zaidi na si dhana nyingine ambazo zilikuwa zikisemwa.

"Kuna maneno yalikuwa yakisemwa kutokana na kambi hizo, wengine wakisema tunafuata mambo ya ushirikina, si kweli, utulivu na umakini wa kujiandaa na mchezo ndio sababu kuu," alisema Madaraka.

Alisema anadhani kwa sasa Simba na Yanga hazikimbii mji, kwa sababu zina wachezaji wengi wageni na ndiyo tegemezi, na wanakuwa hawana usumbufu kwa sababu hawana ndugu na jamaa hapa nchini, hivyo kambi inakuwa tulivyo tofauti na enzi zao.

Simba na Yanga zitakutana katika mchezo huo wa ufunguzi wa msimu mpya baada ya Simba kutwaa taji la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita na kubeba Kombe la Shirikisho, wakati watani zao wao walimaliza kwenye nafasi ya pili kwenye msimamo.

Yanga itashuka kwenye mchezo huo ikiwa na kumbukumbu ya kuondolewa katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Rivers United ya Nigeria wakati Simba yenyewe ikitoka kupoteza mechi ya kirafiki dhidi ya mabingwa wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), TP Mazembe.



Mshambuliaji wa Savana Boys, Mohamed Majili (kulia), akifunga bao huku akizongwa na beki wa Ilala FC katika mechi ya Ligi ya Ufukweni iliyochezwa kwenye Uwanja wa Karume jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Makocha 19 wahitimu Zanzibar*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limesema washiriki 19 wamehitimu kozi ya makocha wa magolikipa katika ngazi ya Daraja la Tatu iliyokuwa inafanyika Visiwani hapa.

Mafunzo hayo yalikuwa ya wiki moja na yalifanyika chini ya Mkufunzi anayetambulika na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Ahmed Machupa.

Kozi hiyo ilishirikisha makocha mbalimbali kutoka Tanzania Bara wanaofundisha timu za Ligi Kuu na Visiwani.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mratibu wa kozi hiyo, Abdul-Mutik Haji, alisema bado mwamko ni mdogo kutoka kwa makocha wa Zanzibar ambao wameshindwa kutumia fursa ya mafunzo hayo na mengine yanayotolewa nje ya Zanzibar.

Haji alisema kati ya washiriki 19 walioshiriki kozi hiyo, alitaja makocha 10 wanatoka Zanzibar na waliobakia walitokea Tanzania Bara.

"Bado baadhi ya makocha wanaendesha shughuli hizi za ukocha kimazoea jambo ambalo wanapaswa kubadilika kwa haraka kwa sababu mpira wa sasa unahitaji makocha wenye elimu tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma," alisema Haji.

Mkufunzi huyo aliongeza wanajipanga kupeleka kozi hiyo, Pemba ili kuwafanya makocha wanaofundisha timu za huko wakidhi sifa zinazotakiwa na CAF.

## Biashara yaipigia hesabu Simba SC

**Na Saada Akida**

LICHA ya timu yake kufanya vyema katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Kocha Mkuu wa Biashara United, Patrick Odhiambo amesema hawezi kuwadharau Simba ambao watakutana katika mchezo wa ufunguzi wa pazia la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2021/22.

Biashara United itawakaribisha mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ifikapo Septemba 28, mwaka huu kwenye Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara.

Timu hiyo inayoshiriki kwa mara ya kwanza mashindano yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), imesonga mbele kwenye michuano ya kimataifa baada ya kuiondoa Dikhil ya Botswana kwa mabao 3-0.

Akizungumza na gazeti hili jana, Odhiambo alisema kufanya vizuri katika mechi za kimataifa haiwafanyi wajione wako bora kuliko Simba na badala yake wanaendelea kujipanga kuhakikisha wanaanza vyema msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Odhiambo alisema anaendelea kuyafanyia kazi mapungufu yaliyoko kwenye kikosi chake ili kujiweka imara zaidi kabla ya kukutana na Simba ambao pia wanashiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Alisema licha ya kushinda mechi zote mbili za Kombe la Shirikisho, ameona mapungufu katika safu ya ulinzi na ushambuliaji.

"Ligi Kuu msimu huu itakuwa na ushindani mkubwa sana, kufanya vizuri kwenye michuano ya kimataifa haitufanyi sisi kujiona ni bora zaidi, tunahitaji kuendelea kujiimarisha na kuboresha sehemu zenye mapungufu katika kikosi chetu," alisema Odhiambo.

Aliongeza ameiangalia Simba na kubaini ina kikosi kizuri kilichotokana na usajili walioufanya, hivyo ni lazima wajipange vyema kuhakikisha wanapata matokeo chanya kwenye mchezo watakaokutana wiki ijayo.

"Simba imefanya usajili mkubwa, ninawaheshimu, ninajua ni timu itakayotupa ushindani, tunajipanga zaidi kwenda kutafuta matokeo mazuri kuanzia mechi hiyo na nyingine zilizopo mbele yetu," alisema Odhiambo.

Naye nahodha wa timu hiyo, Abdulmajid Mungalu aliliambia gazeti hili kikosi chao hakina wasiwasi wowote kuelekea mchezo huo wa kwanza wa ligi kwa sababu wamepata maandalizi mazuri kwa muda mrefu.

"Tumejipanga vizuri kuhakikisha tunapata pointi tatu kwenye uwanja wetu wa nyumbani, mara nyingi huwa hatukubali kufungwa nyumbani," alisema Mangalu.

## ZISIKUPITE

### MARTIAL NJIA MOJA

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Anthony Martial, 25, atakuwa huru kuondoka Manchester United katika dirisha la usajili la Januari. Inaelezwa mchezaji huyo ameitaja Barcelona kama timu mpya anayoweza kujiunga nayo. ***(Eurosport)***

### HENDERSON KUONDOKA

GOLIKIPA wa Manchester United na England, Dean Henderson, 24, anataka uhamisho wa mkopo katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Sun)***

### CHELSEA YAJIPANGA SAWA

CHELSEA wanaandaa ofa mpya ya mkataba wa kiungo wa England, Mason Mount, 22, kiungo wa Ufaransa N'Golo Kante mwenye miaka 30, na kiungo wa Italia, Jorginho (29). ***(Standard)***

### MARQUINHOS ALIKWAMA

CHELSEA walikuwa tayari kutoa euro milioni 100 kwa ajili ya mlinzi wa Paris St-Germain na Brazil, Marquinhos, 27, kipindi cha majira ya joto kilichopita. ***(RMC Spor)***

### LEWANDOWSKI MABAO

MSHAMBULIAJI wa Poland, Robert Lewandowski amesema "sio lazima ajithibitishe katika ligi nyingine" baada ya kushinda tuzo ya mfungaji wa mabao mengi Ulaya kwa kufunga mabao 41 kwenye Bundesliga na Bayern Munich msimu wa 2020-21. ***(Mirror)***

### OYARZABALI ANUKIA CITY

MANCHESTER City inamfuatilia fowadi wa Real Sociedad na Timu ya Taifa ya Hispania, Mikel Oyarzabal, 24. ***(TeamTalk)***

### LENO KUWEKWA SOKONI

ARSENAL itamfanya kipa wa Ujerumani, Bernd Leno, 29, apatikane kwa uhamisho kufuatia ujio wa kipa wa England, Ramsdale mwenye umri wa miaka 23 kwenye klabu hiyo. ***(Eurosport)***

### KOEMAN KUFUKUZWA

BARCELONA wanajiandaa kuachana na kocha mkuu Ronald Koeman, huku bosi wa Ubelgiji, Roberto Martinez akiwa "chaguo bora" kuchukua nafasi ya Mholanzi huyo. ***(Goal)***

### GUARDIOLA NA BARCA

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta hajakata tamaa kujaribu kumshawishi bosi wa Manchester City, Pep Guardiola arejee Nou Camp. Guardiola, 50, aliongoza Barca kushinda mataji matatu ya Ligi ya Hispania. ***(El Nacional)***

### ASENSIO KUONDOKA

WINGA wa Hispania, Marco Asensio, 25, anaweza kuondoka Real Madrid ikiwa hatapewa nafasi zaidi katika kikosi cha kwanza chini ya Carlo Ancelotti msimu huu. ***(Cadena Ser)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HATIMA YA STERLING MASHAKANI ENGLAND

**Ferdinand azitaka Liverpool na United kumsajili mshambuliaji huyo ili...**

**LONDON,** England

MLINZI wa zamani wa Manchester United, Rio Ferdinand amesisitiza klabu za Manchester United na Liverpool zimsajili Raheem Sterling ili kuokoa kipaji chake baada ya mchezaji huyo kuachwa gizani na Manchester City.

Sterling aliisaidia City kutwaa mataji tangu atue Etihad akitokea Liverpool mwaka 2015, lakini muda wake wa kucheza umepunguzwa na Kocha Pep Guardiola. Mchezaji huyo wa kimataifa wa England amecheza mara mbili kwa kuanza katika michezo sita ya City kwenye mashindano yote msimu huu.

> **"Yupo Raheem Sterling, amepoteza kujiamini kwa sababu ameondolewa kwenye timu," alisema Ferdinand kupitia chaneli yake ya FIVE ya Youtube.**

"Kama ningekuwa Liverpool, ningemnunua Sterling hata kesho tu, kama ningekuwa yeye nisingekwenda Barcelona au Real Madrid kwa sasa ndiyo maana nasema Liverpool na United watamchukua.

Sterling amekuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, huku Barcelona na Real Madrid zikitajwa kuwania huduma yake.

Msimu huu unaonekana kuwa mgumu zaidi kwake, kwani hana nafasi ya kucheza mara kwa mara kwenye kikosi hicho.

Sterling alimaliza kama mfungaji bora wa City kwa misimu miwili kwenye Ligi Kuu England akiwa na mabao 20 katika michezo 33 ya EPL, na alizidiwa na Ilkay Gundogan (13) msimu uliopita yeye akiwa amezifumania nyavu mara 10.

MECHI KALI
HOME
AWAY
CADIZ CF
5.35 | 4.20 | 1.59
BARCELONA

1
WEKA PESA.
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4 - WEKA PESA.
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND

2
WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 517,3



# PACQUIAO: SITAPIGANA TENA

**MANILA,** Ufilipino

BONDIA wa Ufilipino, Manny Pacquiao amesema kazi yake ya ubondia imefika tamati ingawa wakuu wa timu yake ya promosheni wameweka wazi mazungumzo ya kustaafu kwa bondia huyo bado.

Bondia huyo mwenye umri wa miaka 42 alipoteza pambano dhidi ya Yordenis Ugas mwezi ulitopita na wengi wakitabiri kwamba huo ndiyo mwisho wake na huenda hilo ndiyo pambano lake la mwisho.

Jumapili Pacquiao alitangaza nia yake ya kuwania urais wa Ufilipino katika uchaguzi utakaofanyika mwakani. Bingwa huyo aliyewahi kutamba mika ya nyuma aliiambia Toni Talks kuwa amemaliza ndondi.

"Kazi yangu ya ndondi tayari imekwisha," Pacquiao alisema.

"Imefanywa kwa sababu nimekuwa kwenye ndondi kwa muda mrefu na familia yangu inasema kuwa inatosha."

Lakini, mkuu wa promosheni wa Pacquiao Sean Gibbons alisema mazungumzo yoyote ya kustaafu bado.

"Seneta ni mgombea wa urais na bado hajafanya uamuzi wowote juu ya maisha yake ya ndondi," Gibbons aliiambia Yahoo Sports.

"Katika wiki chache zijazo atafanya uamuzi wa mwisho ikiwa atakuwa na zaidi au astaafu."



# Messi nje wiki moja

**PARIS,** Ufaransa

LIONEL Messi aliukosa mchezo kati ya Paris Saint Germain dhidi ya Metz uliochezwa kwenye dimba la Saint Symphorien jana kutokana na kuwa majeruhi, imefahamika.

Messi aliyetolewa katika dakika 75 kwenye mchezo wa Jumapili dhidi ya Lyon ambapo Paris walishinda mabao 2-1, huku ikiendeleza mwanzo mzuri, PSG imeshinda mechi sita kwenye ligi huku ikiongoza kwa pointi tano dhidi ya Marseille inayomfuata.

Mshambuliaji huyo ambaye aliacha sintofahamu na kocha wake baada ya kutolewa kwenye dakika ya 75, alifanyiwa vipimo na kukutwa na matatizo ya mfupa wa mguu wake wa kushoto.

Kocha wa PSG, Mauricio Pochettino alisema, "alichukua uamuzi wa kumtoa Messi pale tu, alipohisi kuwa kaumia baada ya kuona akijishika zaidi ya mara moja kwenye kifundo chake."

Taarifa zaidi ilisema nyota huyo wa kimataifa wa Argentina anaweza kuwa nje ya dimba kwa wiki mbili ili kujiugza majeruhi hayo.

Messi hadi sasa bado hajafunga bao lolote tangu atue kwenye Ligi Kuu Ufaransa maarufu 'Ligue I'.

## HABARI MICHEZO


# 350,800 JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 25/09/21 | 17:00 | Leeds vs West Ham | 2.71 | 3.57 | 2.46 |
| 02. 25/09/21 | 17:00 | Watford vs Newcastle | 2.37 | 3.32 | 3.01 |
| 03. 25/09/21 | 17:00 | Blackpool vs Barnsley | 2.52 | 3.31 | 2.66 |
| 04. 25/09/21 | 17:00 | Swansea vs Huddersfield | 2.27 | 3.26 | 3.06 |
| 05. 25/09/21 | 17:00 | Nottingham vs Millwall | 2.81 | 3.05 | 2.56 |
| 06. 25/09/21 | 17:00 | Blackburn vs Cardiff | 2.34 | 3.24 | 2.95 |
| 07. 25/09/21 | 17:15 | Valencia vs Athletic Bilbao | 2.50 | 3.21 | 2.91 |
| 08. 25/09/21 | 18:00 | St Etienne vs Nice | 2.94 | 3.24 | 2.40 |
| 09. 26/09/21 | 15:00 | Mallorca vs Osasuna | 2.91 | 3.06 | 2.61 |
| 10. 26/09/21 | 16:00 | Southampton vs Wolverhampton | 2.57 | 3.22 | 2.82 |
| 11. 26/09/21 | 16:00 | Udinese vs Fiorentina | 2.66 | 3.31 | 2.66 |
| 12. 26/09/21 | 18:30 | Arsenal vs Tottenham | 2.41 | 3.17 | 3.07 |
| 13. 26/09/21 | 19:00 | Lazio vs Roma | 2.75 | 3.65 | 2.39 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 23 - SEPTEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:15 | 3858 | Zenit Izhevsk vs CSKA Moscow | 12.58 | 6.19 | 1.17 |
| 15:00 | 1948 | Hirnik-Sport vs FK Lviv | 6.18 | 3.96 | 1.47 |
| 16:00 | 5525 | Tabor Sezana vs NK Mura | 3.48 | 3.43 | 1.94 |
| 16:00 | 5919 | Acso Filiasi vs UTA Arad | 10.62 | 5.60 | 1.22 |
| 17:00 | 2929 | Prykarpattya Ivano-Frankivsk vs Chernomorets Odessa | 4.54 | 3.53 | 1.69 |
| 17:00 | 5182 | Konyaspor vs Trabzonspor | 3.36 | 3.41 | 2.07 |
| 18:00 | 3669 | Torpedo Vladimir vs Ural Yekaterinburg | 9.50 | 4.55 | 1.30 |
| 18:00 | 5258 | Luka Koper vs NK Aluminij | 1.90 | 3.68 | 3.39 |
| 18:15 | 1947 | Ionikos Nikea FC vs PAS Giannina | 2.62 | 2.91 | 2.86 |
| 18:30 | 1632 | LKS Lodz Pss vs Cracovia | 2.84 | 3.18 | 2.33 |
| 18:45 | 1583 | Ripensia Timisoara vs Dinamo Bucuresti | 3.73 | 3.44 | 1.87 |
| 19:00 | 1254 | BK Frem vs Aarhus | 9.66 | 6.38 | 1.20 |
| 19:00 | 1305 | Horsens vs Silkeborg | 3.10 | 3.44 | 2.07 |
| 19:00 | 1835 | Alliance Lypova Dolyna vs FC Minaj | 2.05 | 3.44 | 3.15 |
| 19:00 | 3088 | LASK Linz vs SV Stripfing | 1.01 | 14.55 | 38.81 |
| 19:30 | 1221 | Sampdoria vs Napoli | 4.22 | 3.82 | 1.80 |
| 19:30 | 5591 | Torino vs Lazio | 3.21 | 3.46 | 2.20 |
| 19:45 | 1670 | Cambuur vs Heracles Almelo | 2.11 | 3.59 | 3.10 |
| 20:00 | 1067 | Fenerbahce vs Giresunspor | 1.39 | 4.64 | 7.11 |
| 20:00 | 2657 | Hammarby vs IFK Goteborg | 1.88 | 3.59 | 3.50 |
| 20:00 | 3620 | Varbergs Bois vs BK Hacken | 2.71 | 3.20 | 2.42 |
| 20:00 | 4475 | Alanyaspor vs Kasimpasa | 1.86 | 3.69 | 3.74 |
| 20:00 | 5250 | Kalmar vs AIK Football | 3.11 | 3.15 | 2.19 |
| 20:00 | 5353 | Mjallby vs Halmstads BK | 2.40 | 3.00 | 2.90 |
| 20:30 | 3208 | Granada vs Real Sociedad | 3.77 | 3.37 | 2.03 |
| 20:30 | 5603 | Osasuna vs Betis | 2.29 | 3.26 | 3.21 |
| 20:30 | 5677 | Volos vs Atromitos | 2.57 | 3.02 | 2.82 |
| 20:45 | 2368 | Alleroed FK vs Brondby | 38.75 | 17.44 | 1.01 |
| 21:15 | 3211 | Maribor vs NK Celje | 1.84 | 3.63 | 3.63 |
| 21:30 | 2442 | Universitatea Craiova vs CFR Cluj | 2.42 | 3.01 | 2.86 |
| 21:30 | 2571 | FC Lugano vs Grasshoppers | 1.92 | 3.40 | 3.84 |
| 21:30 | 3534 | Admira Wacker vs Rapid Vienna | 4.07 | 3.97 | 1.67 |
| 21:30 | 3968 | FC Sion vs FC Luzern | 2.66 | 3.50 | 2.42 |
| 21:30 | 5875 | Slask Wroclaw vs Nieciecza KS | 1.95 | 3.39 | 3.49 |
| 21:45 | 1105 | Dundee Utd vs Hibernian | 3.00 | 3.10 | 2.28 |
| 21:45 | 3268 | Roma vs Udinese | 1.51 | 4.53 | 5.83 |
| 21:45 | 3789 | Anderlecht vs KAA Gent | 2.13 | 3.40 | 3.21 |
| 21:45 | 4233 | Celtic vs Raith Rovers | 1.05 | 9.67 | 23.21 |
| 22:00 | 2605 | Always Ready vs Oriente Petrolero | 1.37 | 4.55 | 6.98 |
| 22:00 | 3133 | Twente vs AZ Alkmaar | 3.30 | 3.55 | 2.04 |
| 22:15 | 1607 | Pacos Ferreira vs Boavista | 2.17 | 3.31 | 3.26 |
| 23:00 | 3704 | Cadiz CF vs Barcelona | 5.35 | 4.20 | 1.59 |

### IJUMAA - 24 - SEPTEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:30 | 4284 | Union San Felipe vs Univ de Concepcion | 2.47 | 3.05 | 2.76 |
| 01:00 | 2863 | CSA AL vs Botafogo RJ | 3.39 | 3.05 | 2.12 |
| 02:30 | 3007 | Jorge Wilstermann vs Independiente Petrolero | 1.53 | 4.50 | 5.40 |
| 03:00 | 4361 | Zacatepec vs Alebrijes De Oaxaca | 1.58 | 3.68 | 5.24 |
| 03:00 | 5302 | Coquimbo vs CD Santa Cruz | 1.99 | 3.19 | 3.58 |
| 03:30 | 1265 | CA Penarol vs Atletico Pr | 2.23 | 2.95 | 3.24 |
| 05:00 | 2608 | CF Pachuca vs Club Necaxa | 1.81 | 3.36 | 4.45 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# ALONSO KUTOPIGA GOTI KUPINGA UBAGUZI



**LONDON,** England

MLINZI wa Chelsea, Marcos Alonso ataacha kupiga goti katika michezo yote inayokuja kwa ajili ya kupinga ubaguzi wa rangi na badala yake kusimama kuonyesha kidole kwenye nembo ya kupinga ubaguzi.

Winga wa Crystal Palace, Wilfred Zaha alikuwa mchezaji wa kwanza kuacha kupiga goti katika Ligi Kuu England na sasa Alonso anaungana naye.

Alonso alinukuliwa akisema, "napinga vikali ubaguzi wa rangi na napinga ubaguzi wa aina yeyote.

"Napendelea kufanya kwa njia hii, na nasema kwa uwazi napinga ubaguzi na namheshimu kila mtu," aliongeza.

Utaratibu wa kupiga goti kabla ya mechi kuchezwa ulianza kipindi cha kampeni ya 'black lives matter' baada ya kusimama kwa Ligi Kuu England kwa siku 100 kutokana na mlipuko wa virusi vya corona mwaka jana.

Alonso amebainisha kupiga goti pekee hakuwezi kumaliza ubaguzi wa rangi na kuongeza kinachotakiwa ni kuwekwa sheria kali ili kila mmoja aheshimiwe.



# Barcelona yashindwa kumfukuza Koeman

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA Ronald Koeman kwa sasa anaendelea kuifundisha Barcelona kwa sababu timu hiyo haiwezi kumfukuza licha ya kuonekana kupoteza mwelekeo.

Barcelona imekuwa kwenye wakati mgumu baada ya kupoteza wachezaji wake muhimu akiwamo Lionel Messi na Antoine Griezmann na hivyo kuwa na matokeo mabaya kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Iwapo hali hiyo itabadilika mwezi ujao kocha mwingine wa zamani Roberto Martinez anatajwa na Bodi ya Barca kuchukua nafasi ya Koeman.

Barcelona haiwezi kumfukuza Koeman mwenye umri wa miaka 58 bila kumlipa karibu pauni milioni 10.

Mwezi ujao ni muhimu kufikiwa uamuzi iwapo Koeman anabaki au anaondoka klabuni hapo.

Barcelona itacheza mechi ya LaLiga ugenini leo dhidi ya Cadiz, halafu itarejea nyumbani Nou Camp Septemba 26, mwaka huu kuwakaribisha Levante.

Barca itakuwa mgeni wa Benfica ifikapo Septemba 29, mwaka huu katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kabla ya kuwavaa mabingwa wa Hispania Athletico Madrid katika La Liga hapo Oktoba 2, mwaka huu.

# Michezo

Alhamisi Septemba 23, 2021

Nipashe



Hatima ya Sterling mashakani England

UKURASA 21



Wachezaji wa Yanga kutoka kushoto, Feisal Salum 'Fei Toto', Kibwana Shomari na Yacouba Sogne wakiwa kwenye mazoezi ya timu hiyo kuelekea katika mechi ya Ngao ya Jamii, mchezo unaotarajiwa kuchezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

## Simba yafikiria makombe

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Didier Gomes amesema kikosi chake hakifikirii mechi moja tu ya Ngao ya Jamii na badala yake kinaendelea kujipanga kutetea makombe yote wanayowashikilia hapa nchini, imefahamika.

Wekundu wa Msimbazi ni mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya nne mfululizo, lakini wanamiliki taji la michuano ya Kombe la FA kwa misimu miwili mfululizo.

Gomes aliliambia gazeti hili jana timu yake imefanya maandalizi kwa ajili ya msimu mzima na si kuangalia mchezo mmoja wa Ngao ya Jamii ambao utachezwa keshokutwa dhidi ya Yanga.

Kocha huyo alisema anajua mechi zote zitakuwa ngumu hivyo watacheza kwa tahadhari na umakini mkubwa.

"Nina imani tutaanza msimu vizuri kwa kushinda taji, tumefanya maandalizi ya kutosha wakati huu, tumejipanga kimbinu na tumeendelea kurekebisha makosa machache, pia tumeboresha maeneo tuliyokuwa bora ili kuhakikisha tunaanza msimu kwa kuchukua taji kama tulivyomaliza msimu kwa kushinda mataji.

"Hakuna mechi rahisi katika haya mashindano na kila timu inafanya maandalizi kusaka ushindi, tunapaswa kuwa makini ili tupate matokeo mazuri ambayo yatatupeleka katika hatua inayofuata," alisema Gomes.

Aliongeza malengo ya Simba ni kufanya vyema zaidi ya ilivyokuwa katika msimu uliopita na kazi ya kwanza itakuwa ni kushinda mechi ya Ngao ya Jamii ili kurahisisha safari ya michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo wataanzia ugenini dhidi ya Biashara United hapo Jumanne.

Baada ya kumaliza Tamasha la Simba Day, mabingwa hao waliendelea na mazoezi kwenye Uwanja wao Bunju ambapo Gomes anashirikiana na Thiery Hitimana na Suleiman Matola.

# Nabi: Yanga tutaweka rekodi

**Na Tunu Hassan, TUDARCo**

## ●●● Afunguka jeshi lake limekamilika na...

WAKATI bundi akionekana kuinyemelea klabu ya Yanga, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Nasreddine Nabi amewaondoa wasiwasi wanachama na mashabiki wa timu hiyo kuelekea mchezo wa Ngao ya Jamii unaotarajiwa kufanyika keshokutwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

**Bundi anaonekana kuizunguka Yanga baada ya kuondolewa katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwenye hatua ya awali na klabu ya Rivers United ya nchini Nigeria, wakifungwa mechi zote mbili huku watani zao, Simba bado hawajaianza safari ya kuwania taji hilo la Afrika.**

Pia ujio wa Ofisa Habari mpya, Haji Manara na fununu za kurejea kwa aliyekuwa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Cedric Kaze, vimetajwa ni moja ya sababu zinazowagawa viongozi, wanachama, mashabiki na baadhi ya wachezaji wa klabu hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema kikosi chake kimeendelea kuimarika na matokeo mabaya waliyopata kwenye michuano ya kimataifa yamesaidia 'kujiuliza' na sasa kila mchezaji yuko tayari kwa vita ya kuwania mataji katika msimu mpya.

Nabi alisema hawako tayari kurudia makosa waliyofanya dhidi ya Rivers United na wanawatahadharisha wapinzani wao, Simba wajiandae kukutana na ushindani katika mchezo huo.

"Tunahitaji kushinda mechi hiyo kuliko kitu kingine kwa sasa, hatukufanya vizuri kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, sasa tumerejea kamili kwenye mashindano ya ndani, tunaanza na Ngao ya Jamii halafu akili na mipango itahamia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara," alisema Nabi.

Aliongeza kupatikana kwa wachezaji wake wa kimataifa ambao aliwakosa kwenye michuano ya CAF, kumekiongezea nguvu kikosi chake na kujiweka imara kuanza kuwania taji hilo la kwanza hapa nyumbani.

"Tuko tayari, tunajua umuhimu wa kupata ushindi Jumamosi, tunataka kuanza na rekodi nzuri katika msimu wa mwaka 2021/2022," Nabi alisema.

Taarifa kutoka Yanga zinasema mazungumzo ya kumrejesha Kaze kwenye kikosi hicho yameshafanyika lakini uamuzi haujatekelezwa kutokana na baadhi ya viongozi kugawanyika.

"Yanga ina makundi manne, hili ni tatizo, hali hii inakwamisha baadhi ya mipango na mikakati kwa sababu hatuzungumzi lugha moja, mbaya zaidi kati yetu kuna wengine wako kimya kabisa," kilisema chanzo chetu.

Wakati huo huo, Katibu wa Baraza la Wazee wa Yanga, Juma Magoma, alisema jijini jana mgawanyiko ulioko ndani ya klabu hiyo ndio unaigharimu timu yao kwa kiwango kikubwa.

"Ninachokiona ni viongozi wa juu kuruhusu hii hali ya makundi ndani ya klabu iendelee kutokea, inatakiwa waliangalie sana, watu hatupewi nafasi ya kutoa maoni yetu ndiyo maana mambo kama haya yanajitokeza, ni mbaya sana," alisema Magoma.

Katika hatua nyingine, Yanga imetajwa kinara wa kuingiza mashabiki wengi katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ikicheza nyumbani kwa msimu uliopita wa 2020/21.

Taarifa iliyotolewa wjana na Shirikisho la Soka Nchini (TFF), ilionyesha Yanga imeingiza mashabiki 141,681 ikicheza nyumbani na kupata kiasi cha Sh. milioni 986.8 wakati watani zao Simba wamekamata nafasi ya pili kwa kuingiza mashabiki 138,518 kwa kujikusanyia Sh. milioni 929.7.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >